# Nipashe

Jumamosi Juni 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581694

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**SON, SPURS MAMBO MAZURI**

UK. 22

**Serikali** yatoa kauli kuhusu maiti kuzuiwa hospitalini



UKURASA 3

**Kibano** zaidi mashirika ya umma utoaji wa gawio

UKURASA 4



**Trump** akutwa na hatia makosa 34 ya uhalifu

UKURASA 17

MIKAKATI 2024/25

# Helikopta kudhibiti wanyamapori wakali

UK. 2



Filamu The Royal Tour, Amazing Tanzania zawekewa mkakati

Meli, matamasha, mechi za Ligi Kuu, utalii tiba

Makumbusho ya Marais kujengwa jijini Dodoma

Majangili maelfu wanaswa, mitego yao yateguliwa

Hoja nzito za CAG zafanyiwa kazi

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ziara ya Makonda yafagia watano

UK.3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mtawala wa Mji wa Serikali wa Sejong, Kim Hyung-ryeol, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Jeshi wa Seoul, Jamhuri ya Korea jana, kwa ajili ya ziara rasmi ya kikazi. **PICHA: IKULU**

## Mafuta ya kula kutoka nje sasa kutozwa kodi zaidi

UKURASA 2

**MICHEZO** SILAHA MPYA YANUKIA SIMBA UK.24

**MAONI,** UK.6



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi (kulia), akisalimiana na Waziri Mkuu mstaafu Frederick Sumaye, Mjini Katesh, Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara jana, kabla ya kwenda kwenye mkutano wa hadhara akitokea kwenye ziara yake mkoani Singida. **PICHA: ROMANA MALLYA**

MIKAKATI 2024/25

# Helikopta kudhibiti wanyamapori wakali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI itanunua helikopita mbili kwa gharama ya Sh. bilioni 45.2 mwaka ujao wa fedha ili kukabiliana na wanyamapori waharibifu wanaovamia makazi ya wananchi.

Hatua hiyo ni sehemu ya mikakati ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuboresha na kuinua sekta za utalii na uhifadhi nchini.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, akiwasilisha bungeni jijini hapa jana makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, alisema ununuzi wa helikopta hizo utafanywa kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Alisema kuwa katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori waharibifu, pia watachimba mabwawa 30 kupitia TANAPA (12), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) itakayochimba mawili na TWPF (16).

"Mabwawa hayo yatachimbwa katika Hifadhi za Taifa Serengeti (5), Ruaha (1), Tarangire (2), Katavi (2), Nyerere (2), Saadani (2), Mikumi (2) na Mkomazi (3) na Mapori ya Akiba Rungwa (2), Kizigo (2), Selous-Liwale (2), Muhesi (2), Maswa (2) na Msanjesi (1)," alisema Angellah.

Waziri alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Mei mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 2.4 zimelipwa kwa wananchi 10,552 waliopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya 48. "Wizara pia imefanya mapitio ya Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 kwa kuongeza viwango vya malipo kwa asilimia 50 kwa matukio ya majeraha ya muda, uharibifu wa mazao na vifo vya mifugo na asilimia 100 kwa majeraha ya kudumu na vifo," alisema.

Waziri huyo pia alisema watatekeleza ujenzi wa Makumbusho ya Marais - Dodoma, ukilenga kuongeza wigo katika uhifadhi wa urithi wa asili na utamaduni wa Mtanzania.

Alisema mradi huo pia una lengo la kuhifadhi historia za waasisi na viongozi wakuu wa nchi, kuimarisha na kuhamasisha utafiti wa masuala ya historia na kuongeza vivutio vya utalii vya utamaduni.

"Kwa mwaka wa fedha 2024/25, ujenzi huu utatekelezwa na fedha za ndani kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makumbusho ya Marais wa Tanzania, jijini Dodoma," alisema.

**VIPAUMBELE**

Waziri Angellah aliwasilisha vipaumbele vinane vya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25, vikijikita katika kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Hivyo ni pamoja na mwendelezo wa programu maalum ya Tanzania - The Royal Tour, filamu ya Amazing Tanzania pamoja na mikakati mingine mikubwa kupitia matangazo katika ligi kuu za michezo mashuhuri duniani.

Mkakati mwingine kwa mujibu wa waziri huyo ni kufanya matangazo kwenye ndege, misafara ya utangazaji utalii, matamasha makubwa ya kimataifa na mitandao mbalimbali ya kimataifa na vyombo vya habari, kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, ikiwamo maeneo ya malikale pamoja na utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, tiba na utamaduni.

Waziri Angellah alisema jukumu jingine ni kuboresha miundombinu katika maeneo ya hifadhi ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika.

"Wizara itaimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale. Pia itatekeleza mipango na mikakati ya uhifadhi pamoja na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa thamani ya mazao ya misitu na nyuki, kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na malikale," alisema.

Aliongeza kuwa wizara yake itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji takwimu na kufanya utafiti wa kimkakati na kutoa huduma za ushauri zinazohusu masuala ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori, misitu na nyuki, malikale na uendelezaji utalii.

Waziri huyo pia alisema wataendeleza mikakati ya kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi na mifumo ya ukusanyaji mapato na fedha za kigeni.

**MAFANIKIO**

Kuhusu mafanikio, Waziri Angellah alisema idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa asilimia 96 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi watalii 1,808,205 mwaka 2023.

Alibainisha kuwa idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa asilimia 152 kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia 1,985,707 mwaka 2023.

"Mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.4 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 161 kwa watalii wa kimataifa.

"Mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka Sh. bilioni 46.3 mwaka 2021 hadi Sh. bilioni 175.3 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 279," alibainisha waziri huyo.

Alisema kuwa ili kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori, wizara kupitia taasisi zake za uhifadhi itaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na ujangili wa mwaka 2023-2033 na mkakati wa kusimamia na kuhifadhi tembo nchini wa mwaka 2023-2033.

Alisema utekelezaji wa mikakati hiyo utawezesha udhibiti wa matukio ya ujangili na biashara haramu ya nyara nchini.

Waziri huyo pia alieleza mafanikio waliyopata katika kukabiliana na matukio ya moto na ujangili, ambayo ni sehemu ya hoja zilizotawala ripoti za mbili za 200/21 na 2021/22) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umeanza kutumia teknolojia za kisasa, ikiwamo ndege nyuki (drone) kwa lengo la kupata taarifa za matukio mbalimbali katika hifadhi za misitu.

Kupitia doria hizo, Waziri Angellah alisema jumla ya watuhumiwa 1,223 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikiwamo kutaifishwa kwa magunia 21,596 ya mkaa uliovunwa bila kufuata utaratibu, mbao 24,036 zenye mita za ujazo 1,498, kuni zenye mita za ujazo 90 na magogo 1,256 yenye mita za ujazo 415, mifugo 12,694, pikipiki 1,514, magari 149 na vyombo vya majini (7).

# Mafuta ya kula toka nje kutozwa kodi

**Na Romana Mallya,** SINGIDA

SERIKALI imesema inaweka kodi katika mafuta ya kupikia yanayoagizwa kutoka nje ili kulinda mazao ya bidhaa hiyo hasa alizeti kwa lengo la kukuza hali za maisha ya wakulima nchini.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, aliposimamishwa na wananchi katika eneo la Itaja, Wilaya ya Singida wakati akiendelea na ziara yake ya kuzungukia mikoa mitano, akihitimisha Singida na kwenda Manyara.

Akiwa eneo hilo, baada ya kusikiliza kero za wananchi waliomsimamisha, Balozi Nchimbi alimpigia simu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ili kutoa ufafanuzi wa maeneo yanayohusu sekta yake.

Katika ufafanuzi wake, Waziri Bashe alisema serikali itaendelea kulinda zao la alizeti pamoja na wakulima nchini.

"(Wananchi) waendelee kusikiliza bajeti ya Waziri wa Fedha kesho kutwa, tunaweka kodi kwenye mafuta yanayotoka nje ili kuwalinda wakulima wa zao hili. Haya ndiyo maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi (CCM)," alisema Bashe.

Baada ya maelezo hayo, Balozi Nchimbi alishukuru kwa maelekezo ya Rais Samia ambayo alitafsiri kwamba yatainua kilimo cha alizeti na kukuza hali ya maisha ya wakulima wa Singida na Tanzania nzima.

"Tutaendelea kusimamia kama alivyosema Waziri kuhakikisha kwamba, mazao yanayotokana na alizeti yanapatikana kwa haraka, yanapangiwa bei nzuri ili wakulima kipato chao kiongezeke," alisema.

Dk. Nchimbi alimweleza waziri huyo kuwa kuna changamoto mbili ambazo wananchi wamezitoa, moja soko la mazao ambapo tayari eneo wameshalitayarisha, hivyo Katibu Mkuu akaelekeza likamilike kabla ya uchaguzi.

Baada ya maelekezo hayo, Waziri Bashe alisema mkoa huo wanazalisha vitunguu, hivyo atatuma wataalam kuanzia Jumatatu kwenda hapo.

"Mheshimiwa Katibu Mkuu, ninajua hapo atakuwapo Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya watakuwapo hapo, eneo linalojengwa soko, ninaamini ni soko la vitunguu tu, ndio hitaji lao kubwa.

"Kwa hiyo tutakachokiomba eneo lile lipimwe liwe na hati inayojitegemea na hati hiyo iandikwe Halmashauri ya Singida Vijijini na Wizara ya Kilimo, iandikwe kwa majina mawili ili kesho na kesho kutwa Baraza la Madiwani wasije kubadilisha matumizi ya eneo," alisema.

Bashe alisema watapeleka wataalam hao na soko hilo litajengwa kabla ya kufikia uchaguzi mkuu.

Katika jambo la pili, Balozi Nchimbi alimweleza Waziri huyo kuwa Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhan Ighondo, amezungumzia kuhusu mradi wa umwagiliaji (mradi wa Msangi) na Bashe akafafanua kuwa mipango inakwenda vizuri na una thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 10 na tayari mkandarasi ameshapatikana na kwamba utakamilika kabla ya uchaguzi mkuu.

Akijibu kero nyingine za wananchi zilizotolewa hapo za sekta ya afya, Balozi Nchimbi alielekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha kunajengwa Kituo cha Afya cha Ndimu na ujenzi wake uanze mara moja ifikapo Agosti 15, mwaka huu.

## HABARI KITAIFA

# Ziara ya Makonda yafagia vigogo watano

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameagiza kuhamishwa kazi kwa watumishi watano walioko kwenye idara na vitengo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha kutokana na kukaa muda mrefu na kukwamisha baadhi ya miradi ya maendeleo.

Kadhalika, Makonda ameagiza kushushwa vyeo Ofisa Elimu Msingi, Hussein Bakari na Ofisa Elimu wa Sekondari, Yusuph Mange.

Makonda alifikia hatua hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi katika viwanja vya Kilombero jijini Arusha huku akisema kuna miradi mingi imekwamishwa pasipo sababu za msingi na hawako tayari kuwavumilia watendaji wazembe.

Aidha, Makonda alimtaka Mkurugenzi wa Jiji, Mhandisi Juma Hamsini, kueleza watumishi ambao wanakwamisha miradi ya maendeleo akamjulisha waliofanya kazi kwa zaidi ya miaka mitano katika kituo kimoja cha kazi wahamishwe.

"Wakuu wa idara ambao ni zaidi ya miaka mitano niwatakie kila la heri na utaratibu wenu utaandaliwa na Katibu Tawala wa Mkoa. Si kwamba nawachukia, hiki kibarua si chetu ni cha wananchi na wale ambao wa msingi na sekondari mnapotoka katika huu uwanja si wakuu wa idara na kama mna magari myakabidhi kwa mkurugenzi," alisema.

Mkonda alisema wafanyakazi waliobaki sasa ni wakati wa kufunga mkanda watapitia kila mkuu wa idara kuangalia utendaji wa kazi. Alisema ili kuwajibika kwa Pamoja, kila mmoja anatakiwa kusimama katika nafasi yake ikiwamo kutatua kero za wananchi.

Aidha, Makonda alisema kuna fedha ambazo zimeshindikana kutumika matokeo yake wanafunzi wanakosa matundu ya choo, madarasa na mabwalo.

"Si kwa sababu fedha hakuna ni mtu mmoja ameamua kukaa kimya, hii ndio tafsiri yake. Hatuwezi kufanya kazi kwa aina hii. Ujenzi wa shule ya ghorofa na matundu ya choo ifikapo Juni inatakiwa iwe imekamilika. Zabuni ilikosa mzabuni na kurudiwa kutangazwa upya mara ya pili na thamni yake ni Sh. milioni 240. Fedha zipo mradi haujaanza," alibainisha.

Alisema maboresho ya ujenzi wa Shule ya msingi Imara yanayogharimu Sh. milioni 16, mradi haujaanza kutekelezwa na idara ya elimu ya msingi haijawasilisha vinavyotakiwa idara ya ununuzi.

"Sh. milioni 25 ujenzi wa vyoo vya Shule ya Msingi Kijenge hakuna kilichofanyika kwa sababu idara ya msingi haijapeleka mahitaji kwenye idara ya ununuzi. Ukarabati wa madarasa manne katika shule za msingi Matebesi, Nanenane, Ngarenaro na Makumbusho, yote hii miradi haijakamilika na fedha zipo lakini hazijatumika," alisema.

Makonda, baada ya kusema hayo, aliwaita maofisa elimu hao huku akieleza maabara hazijajengwa, ujenzi wa bwalo lenye thamani ya Sh. milioni 80 hakuna kilichoendelea na miradi mingi imekwama na kusababisha changamoto kwa wanafunzi.

"Kuna watu wanalipwa mishahara tena ni mikubwa na watoto wanaamini hatuna fedha kumbe ipo ila ni uzembe wa watu kutowasilisha mahitaji kwa idara ya ununuzi. Kila sehemu hakuna palipoanza kisa idara ya elimu haijawasilisha taarifa.

"Nyie si ndio mnawasimamia watoto wetu? Kuanzia leo (juzi) nyie si wakuu wa idara zenu. Andikeni barua wenyewe mmwambie Katibu Mkuu kuwa mkuu wa mkoa ametuambia kutokana na uzembe na kushindwa kusimamia idara zetu kumesababisha watoto wa Jiji la Arusha kukosa matundu, madarasa na stahiki zao zote ikiwamo maabara hatufai kuwa wakuu wa idara. Tumeelewana ... tumemalizana," alisema.

Makonda alisema kwa cheo chao hawalipwi mshahara peke yake wanapewa na fedha za mawasiliano, usafiri na posho yao hailingani na mwalimu wa kawaida.

# Serikali yatoa kauli hospitali kuzuia maiti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema imeshatoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kutozuia maiti na kuweka utaratibu wa kulipa gharama za matibabu na madeni ya miili ya marehemu.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Segerea, Bonnah Kamoli (CCM), aliyehoji kama ni kweli kauli ya serikali kwa hospitali kutozuia maiti kwa sababu ya deni la matibabu ni ya kisiasa.

Dk. Mollel alisema serikali ilishatoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kupitia waraka namba moja wa mwaka 2021 wa kutozuia maiti na kuweka utaratibu wa kulipia gharama za matibabu na madeni ya miili.

"Nitoe rai kwa waganga wakuu wa mikoa, wilaya na waganga wafawidhi wa hospitali kwa ngazi zote nchini kuzingatia maelekezo ya mwongozo huu na kuhakikisha wananchi wanapata huduma pasipo kuwapo vikwazo vinavyochelewesha marehemu kuzikwa," alisema.

Katika swali lake la nyongeza, Kamoli alihoji kama serikali haioni kuna haja ya kuharakisha mchakato wa bima ya afya kwa wote ili wananchi kuondokana na tatizo la maiti kuzuiwa kutokana na gharama za matibabu.

Dk. Mollel alisema waganga wakuu wa mikoa, wilaya na waganga wafawidhi wa hospitali kwa ngazi zote nchini wanatakiwa kuujua mwongozo huo na kuufanyia kazi.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian




Kazi ya upanuzi wa barabara ya Morogoro kuanzia Kimara Mwisho hadi Ubungo, ikiendelea katika eneo la Korogwe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kibano zaidi gawio mashirika ya umma

**Na Maulid Mmbaga**

MSAJILI wa Hazina, Nehemia Mchechu (pichani), amesema kisheria kila shirika la umma linatakiwa kuwa na mrejesho wa mtaji usiopungua asilimia tano na kwamba sheria hiyo inawataka waisimamie kwa kina na kuhakikisha kila shirika linatekeleza wajibu huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, pembeni ya kikao cha mwaka cha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mchechu alisema hawatakuwa na mzaha katika kusimamia suala hilo ili kufanikisha malengo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyetaka makusanyo yasiyo ya kikodi yafike asilimia 10 ya makusanyo ya kodi.

Mchechu alisema mwaka huu TADB imepeleka gawio serikalini la Sh. milioni 850 huku akibainisha kuwa mwaka ujao wa fedha, benki hiyo inatarajiwa kuongezewa zaidi ya Sh. bilioni 100 kama mtaji na kwamba wameitaka kuweka sera ya urejeshwaji wa faida kwa sababu serikali inataka iendelee kutoa huduma kwa wananchi kupitia mapato hayo.

"Gawio hili litasaidia huduma za serikali na katika suala hilo kwa kweli tutakuwa wakali zaidi. Kila shirika la umma lazima lijitahidi kuwa na marejesho ya mtaji isiyopungua asilimia tano na sheria hiyo tutaisimamia kwa kina na kuhakikisha kila shirika linafanya hivyo.

"Mwaka huu tunafikiri malengo yetu tutayatimiza ya kufikia makusanyo ya Sh. trilioni moja na tunakoenda tunataka lengo hilo liongezeke kwa malengo ambayo Rais alitaka kwa kipindi cha miaka mitano makusanyo yasiyo ya kikodi yafikie asilimia 10 ya makusanyo yasiyo ya kikodi na hakuna taasisi itakayoachwa iendelee kuchechemea," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema benki hiyo iliyoanzishwa kwa kusudi maalumu la kuwasaidia wakulima inaendelea kukua na kwamba mwaka 2023 mtaji uliongezeka kutoka Sh. bilioni 448 hadi bilioni 607 na kutengeneza faida ya kabla ya kodi takribani Sh. bilioni 19.

Pia alisema mwaka huu serikali imeipatia TADB Sh. bilioni 170 kwa lengo la kuiongezea mtaji, jambo linaloisaidia kuendelea kutekeleza wajibu wake wa kuwasaidia wakulima kubadilisha kilimo chao kutoka cha kujikimu hadi kuwa cha kibiashara.



"Nia yetu ni kuleta maendeleo kwa wananchi kupitia sekta ya kilimo, kwahiyo pale ambako tutaona wakulima wetu wamepata changamoto ikiwemo mafuriko tunachukua hatua za kuona ni jinsi gani tunaweza kushirikiana nao kuhakikisha kwamba wanarudi shambani," alisema Nyabundege.

# Mbaroni tuhuma za mauaji, kusafirisha dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha linamshikilia Peter Mwacha (18) dereva bajaji, mkazi wa Sombetini jijini Arusha kwa madai ya kusafirisha dawa za kulevya.

Sambamba na Mwacha. Jeshi hilo pia limemkamata mtuhumiwa wa mauaji.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 29, mwaka huu, saa 8:22 mchana katika maeneo ya Elerai jijini hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Justine Masejo, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa na mabunda 316 yenye uzito wa kilogramu 98.55.

Alisema mtuhumiwa huyo alikuwa anasafirisha dawa hizo kwa kutumia bajaji yenye namba za usajili MC 541 CXL aina ya TVS huku akibainisha kuwa taratibu zingine za jeshi hilo zinakamilishwa ili mtuhumiwa afikishwe katika vyombo vya sheria.

Kamanda Masejo alisema katika tukio lingine, jeshi hilo limemkamata mtuhumiwa wa mauaji, Ramadhan Yahaya (28), maarufu kwa jina la Msambaa, kwa madai ya kuhusika katika tukio la mauaji yaliyofanyika Mei, mwaka huu, eneo la Daraja Mbili, jijini Arusha.

SACP Masejo alibainisha kuwa hali ya jiji la Arusha ni shwari ingawa yapo matukio madogo madogo ambayo wahalifu waliotenda wanaendelea kukamatwa kama alivyokamatwa mtuhumiwa huyo aliyekimbilia jijini Dodoma baada ya kutenda tukio hilo.

Ametoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi mkoani humo kwa kutoa taarifa za kweli za kihalifu kwenye vyombo vya dola au serikali za mitaa.

Pia aliwataka wananchi kutokutoa taarifa kwenye mitandao zisizo za kweli na kwamba hali hiyo inasababisha wahalifu kukimbia na kukwepa mkono wa sheria ikiwa ni pamoja na kuibua taharuki na hofu kwa wakazi na wageni wanaotembelea mkoa huo.

# Mpango asisitiza unafuu gharama gesi

**Na Joseph Mwendapole**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amezitaka kampuni zinazouza mitungi ya gesi kupunguza gharama ili kuwawezesha Watanzania wengi maskini wamudu kutumia nishati hiyo ikiwa ni hatua ya kunusuru uharibifu wa mazingira.

Amezitaka kampuni hizo pia kusambaza mitungi hiyo maeneo yote ya vijijini ili kuwafikia wananchi wengi badala ya kujikita kwenye miji pekee.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la wadau wa mazingira lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikisha na wadau mbalimbali wa mazingira.

Dk. Mpango alisema Siku ya Mazingira Duniani inajielekeza kwenye urejelezaji wa ardhi ili kukabiliana na jangwa na ustahimilifu dhidi ya ukame.

"Kaulimbiu hii inatutaka kurejesha ubora wa ardhi kama sehemu ya kukabiliana na jangwa na ajenda hii ni muhimu kuitafakari kwa kina kwa sababu sehemu kubwa ya baadhi ya mikoa yetu imeshakuwa nusu jangwa. Mpaka sasa mikoa iliyoathirika sana ni Mwanza, Shinyanga, Arusha, Tabora, Dodoma, Singida na Kilimanjaro katika wilaya za Same na Mwanga," alisema.

Alisema kama hatua madhubuti hazitachukuliwa kuokoa mazingira, Tanzania itakuwa inapoteza wastani wa asilimia tatu ya pato la taifa kwa mwaka ifikapo mwaka 2030 kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Makamu wa Rais alisema washiriki wa kongamano hilo wanapaswa kusaidia kuandaa mikakati mbalimbali ya kutatua changaoto za mazingira kwa kuwa Tanzania imejaaliwa kuwa na mazingira bora yaliyojaa viumbe hai kama wanyamapori, ndege wa aina mbalimbali, misitu mikubwa ambavyo vyote vinahitaji kulindwa kwa malsahi ya vizazi vijavyo.

"Ni jambo la kusikitisha kuona shughuli za binadamu za kujitafutia kipato mienendo yetu haizingatii sheria na kwa kiasi kikubwa tunafuga kwa kuhamahama, tunavuna misitu na kuchoma misitu ovyo, ujangili, uvuvi haramu na wa kutumia baruti na kutupa taka taka ovyo na kutiririsha majitaka sumu," alisema.

Tanzania na dunia kwa sasa, alisema inakabiliwa na athari zitokanazo na uharibifu wa maingira kama joto kali, kimbunga, mafuriko na maporomoko ya ardhi, vifo vya binadamu na mifugo, ukame uliopitiliza, kuongezeka kwa kina cha bahari na baadhi ya viumbe na mimea kufa, kuibuka kwa magonjwa mbalimbali ya wanayama na mimea.

"Hivi karibuni tumeshuhudia madhara makubwa ya mabadiliko ya tabia nchi ambapo mvua kubwa ilinyesha na kusababisha mafuriko ambapo baadhi ya watu walikufa na wengine kupoteza makazi, barabara, nguzo za umeme na majengo ya serikali yaliharibiwa na asilimia moja ya pato la taifa itaendelea kupotea kila mwaka kama hatutachukua hatua," alisema.

Makamu wa Rais pia aliagiza machapisho yote yenye taarifa za mazingira yawe kwa kiswahili na kingereza ili watanzania wengi ambao ndio walengwa waweze kupata taarifa.

"Kama tunataka wadau wetu wa maendeleo nao wajue basi tuweke kwenye lugha zote mbili ya kingereza na Kiswahili kwa hiyo naagiza kuanzia sasa machapisho yote yawekwe kwenye lugha hizo," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema hilo ni kongamano la sita kufanyika kuelekea siku ya mazingira duniani.

Alisema uharibifu wa mazingira umesababisha nchi nyingi za kusini mwa Afrika kuwa na kiwango kikubwa cha ukame hasa nchi za Angola, Botswana, Namibia na Afrika Kusini ambako kwenye baadhi ya maeneo yao wanyama wanakosa hata maji ya kunywa.

Jafo alisema mashariki mwa Afrika, Tanzania, Kenya, Somalia na Ethiopia zilishuhudiwa mvua nyingi ambazo zimesababisha vifo vya watu na mifugo na watu wengi kukosa makazi kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Alisema ofisi yake ilijiwekea lengo la kuhakikisha inapanda miti milioni 276 na kwamba taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa wameshafanikiwa kupanda miti milioni 266 sawa na asilimia 79.3.

"Tunatekeleza mradi mkubwa wa mazingira katika mikoa ya Njombe, Iringa Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi kwa kurejesha maeneo yaliyokuwa yameathirika na ukame lakini kwenye maeneo mengi hasa Rukwa kwenye bonde la Lyamba Lyamfipa hali imeanza kuwa nzuri sana," alisema.

# Waziri Mkuu aagiza kuanzishwa majukwaa ubunifu halmashauri

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amezitaka halmashauri zote nchini kukamilisha uanzishwaji wa madawati ya sayansi, teknolojia na ubunifu ifikapo Julai, mwakani.

Pia ameziagiza halmashauri kuhakikisha masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu yanakuwa sehemu ya mipango na bajeti za kila mwaka ili kuwahudumia vijana wanaojishughulisha na masuala ya ubunifu na kwamba kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana katika maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 2024, yanayofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal jijini Tanga. Maadhimisho hayo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya kuongeza hamasa ya kukuza elimu, ujuzi na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Kadhalika alizitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ifikapo Julai, mwakani, shule zote za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na maendeleo ya wananchi viwe vimeanzisha majukwaa ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Alisema serikali inaendeleza kazi 283 za ubunifu zilizotokana na Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

"Tayari bunifu 42 kati ya hizo zimeshaingia sokoni na imewezesha kuanzishwa kwa kampuni 94 kutokana na bunifu na teknolojia zinazobuniwa na wabunifu wa Kitanzania.

Nitoe wito kwa wabunifu nchini, mmebuni kazi na kazi hizo zinamatokeo, jipangeni kuboresha kazi zenu, fungueni kampuni na mtangaze bidhaa hizo," alisema.

Majaliwa pia alisema serikali imeanzisha vituo vya umahiri 12 katika taasisi za elimu ya juu na taasisi za utafiti na maendeleo nchini.

"Vituo hivyo vimeanzishwa kwa lengo la kuchagiza utafiti, ubunifu na ubiasharishaji wa matokeo yanayotokana na shughuli hizo," alisema.

Majaliwa alizitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI kuweka mfumo mzuri wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na mitaala iliyoboreshwa ili kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali yanafikiwa.

Alisema serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi miundombinu ya kutolea elimu katika ngazi zote za elimu nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema wizara inaendelea na hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha fursa na ubora wa elimu nchini kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia zingine za kufundishia na kujifunzia.

"Mifano ya hatua hizo ni pamoja na mkakati wa taifa juu ya matumizi ya teknolojia za kidigitali katika elimu, utoaji wa mafunzo kabilishi kwa walimu na mradi wa`Smartwasomi` ambao utajumuisha kuanzisha madarasa janja (smartclasses) yanayotoa fursa ya kufundisha wanafunzi katika maeneo tofauti kwa wakati mmoja"

Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu ni matokeo yauunganishwaji wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Ubunifu na Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, yaliyokuwa yanaratibiwa na Wizara, Maonesho ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi yaliyokuwa yanaratibiwa na NACTVET na Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyokuwa yanaratibiwa na TCU.



Mwendesha baiskeli ya magurudumu matatu maarufu guta, akiwa amepakia mzigo wa miwa na abiria juu, katika barabara ya Uhuru, eneo la Karume jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo kinachovunja sheria za usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mke, hawara mbaroni tuhuma mauaji mume

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia mke na anayedaiwa kuwa ni hawara yake kwa tuhuma za mauji ya mume wake.

Watuhumiwa hao ambao majina yao yamehifadhiwa kwa kuwa wako kwenye uchunguzi, wanadaiwa kuhusika na kifo cha Victor Mwakapesa (41) mkazi wa Ilembo, mjini Vwawa, Mbozi kisha mwili wake kuutupa katika msitu wa Ipoloto, wilayani Mbeya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Augustino Senga, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo amesema uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi.

Kamanda Senga alisema Mwakapesa alitoweka nyumbani tangu Aprili 30, mwaka huu, akiwa na mke wake kabla ya mwili wake kuokotwa Mei 9, mwaka huu, ukiwa umetupwa katika msitu wa Mpoloto.

Alisema mpaka sasa wanawashikilia watu wawili wanaosadikiwa kuhusika na tukio hilo akiwemo mke wa marehemu ambaye ni mtumishi wa serikali (muuguzi) katika moja ya vituo vya kutolea huduma za afya wilayani Mbozi. Alisema mwingine anayeshikiliwa kuwa ni kijana ambaye ni dereva bodaboda.

"Tunawashikilia watu wawili akiwemo mke wa marehemu kwa kuwa mara ya mwisho yeye ndiye alikuwa na mumewe (marehemu)," alisema.

Kamanda Senga amesema taarifa za mwili wa marehemu kuokotwa katika msitu wa Ipoloto zilitolewa Mei 9, mwaka huu, katika kituo cha polisi Mbalizi, mkoani Mbeya na ulichukuliwa na kwenda kuhifadhiwa katika Hospitali ya Ifisi, mkoani Mbeya.

Alisema Mei 29, mwaka huu, ndugu wa marehemu walipata taarifa na kwenda katika hospitali hiyo kisha kumtambua marehemu.

"Mwakapesa alikutwa na majeraha mbalimbali katika mwili wake ikiwamo majeraha makubwa kichwani na jicho moja kuvimba hadi kutoka," alisema.

# Kamati yapendekeza mambo matatu uendeshaji treni ya SGR kwa faida

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Usimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) inayoongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, imetoa mapendekezo matatu ya kuwashirikisha wadau muhimu ili kuhakikisha lengo la mradi huo linafikiwa huduma zinapoanza.

Mapendekezo hayo yalitolewa juzi baada ya kamati hiyo kuhitimisha ziara ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro iliyokuwa na lengo la kukagua miundombinu hiyo na kufanya kikao kifupi na bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwenye stesheni ya Morogoro.

Prof. Kahyarara alisema mapendekezo hayo yalilenga uendeshaji wa mradi huo utakavyoleta faida, utakavyofanya kazi na sekta zingine za uzalishaji zinavyoweza kuchangia katika mradi huo. Aliwataja baadhi ya wadau watakaoshirikishwa kuwa ni kutoka sekta ya kilimo, vyombo vya ulinzi na usalama, viwanda, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na wafanyabiashara binafsi.

Kwa mujibu wa Prof. Kahyarara, lengo la kuhusisha vyombo vya ulinzi na usalama ni kuhakikisha usalama mradi, watu na mali zao unakuwa wa uhakika.

"Bila kuimarisha shughuli za kiuchumi kwa kushirikisha wadau wakuu, lengo la serikali la kuwa na mradi huu (SGR) haliwezi kufikiwa kwa urahisi. Ushirikishwaji wa wadau ni njia rahisi yenye ufanisi na yenye kuweka mazingira bora ya uendeshaji wa mradi," alisema.

Prof. Kahyarara aliongeza kuwa ushirikishwaji wa wadau utasaidia serikali kutambua masuala muhimu na kuandaa mikakati madhubuti na yenye tija.

Alisema mpango wa baadaye ni kuona wananchi wanaoishi pembezoni mwa njia ya reli wanatumia fursa hiyo kwa kutumia huduma zake kusafirisha mazao na bidhaa za mashambani na kuepukana na hasara za mazao yao kuharibika njiani kwa kuchelewa kufika sokoni.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Lawrence Mafuru, alisema sekta ya uchukuzi ina mchango mkubwa katika kuchochea sekta nyingine za kilimo na viwanda kufanya vizuri kwani bila kuwa na sekta mahiri ya usafiri, haitakuwa rahisi kufikia lengo lililokusudiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema menejimenti iko kwenye mazungumzo na taasisi za fedha ili kuibua mbinu nzuri ya utoaji wa tiketi kwa ajili ya kuepuka upotevu wa mapato na usumbufu kwa abiria.

Alisema TRC inakamilisha mifumo, ikiwamo usimamizi wa mizigo na ukataji tiketi na kwamba hata watumiaji wa simu za 'kitochi' watakuwa na uwezo wa kukata tiketi kidigitali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fainali FA CUP iwe darasa kwa timu zote zilizoshiriki

**FAINALI** ya mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la FA inatarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa New Amaan Complex ulioko Zanzibar.

Mechi hiyo itawakutanisha mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Yanga dhidi ya Azam FC, zote kutoka Dar es Salaam.

Awali fainali hizo zilipangwa kufanyika kwenye Uwanja wa Tanzanite ulioko katika Mji wa Babati mkoani Manyara lakini kwa sababu ya miundombinu ya uwanja huo kutokuwa rafiki, Shirikisho la Soka Nchini (TFF), liliamua kuhamishia mchezo huo Zanzibar.

Kumalizika kwa fainali hiyo, ndio kufungwa rasmi kwa msimu wa soka Tanzania, ikiwa zimepita siku tano tu pazia la Ligi Kuu Bara limefungwa na Yanga kutetea ubingwa kwa msimu wa tatu mfululizo.

Yanga na Azam hazijafika katika hatua hiyo kwa kubahatisha, ni kutokana na kuwa na kikosi pamoja na benchi la ufundi imara ambalo limekuwa likifanya vyema kazi yake kuanzia msimu huu ulipofunguliwa hapo Agosti mwaka jana.

Timu hizo mbili ndio zilizomaliza pia katika nafasi mbili za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ikitwaa ubingwa na Azam FC ikimaliza kwenye nafasi ya pili baada ya kuizidi Simba idadi ya mabao ya kufunga, hakika ilikuwa ni vita nyingine 'kali' msimu huu huku pia timu nyingine zikipambana kujinusuru kushuka daraja. Mechi hiyo mbali na kuipa heshima timu itakayofanya vizuri kwa kubeba kombe hilo lililoanzishwa maalumu kupata mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini itatoa taswira halisi ya kikosi kilichoandaliwa kuonyesha ushindani katika kila mchezo.

Yanga na Azam zimekuwa zikionyesha soka safi msimu huu, kila mechi kwao ikionekana ni fainali, kwa sababu kwa wachezaji, benchi la ufundi, viongozi, wanachama na mashabiki wake walifanananisha na fainali ili kujihakikishia wanashinda na kujiimarisha kwenye mbio walizokuwa wanashindana.

Hii ilionekana hata pale Yanga ilipotolewa katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na vigogo wa Afrika Kusini, Mamelodi Sundowns, haikuwa mechi rahisi kwa kila upande, vijana wa Miguel Gamondi, walionekana na kiu ya kutaka kushinda kila taji.

Azam FC pia kwa upande wao, licha ya kuteleza katika baadhi ya michezo ikiwamo kukubali kichapo kutoka kwa Namungo FC wakiwa nyumbani kwao Azam Complex, waliendelea kupambana kusaka pointi muhimu na hatimaye kutimiza malengo yao ya kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao. Timu nyingine zote zilizoshiriki michuano ya Kombe la FA kuanzia ngazi ya wilaya zinatakiwa kujitathmini na kurekebisha pale ilipokosea ili msimu mpya wa mashindano hayo utakapoanza wafanye vyema na kuongeza ushindani.

Kama tunavyoshuhudia katika mataifa yaliyoendelea, katika hatua ya robo fainali, nusu fainali au tunashuhudia fainali za michuano ya FA hushirikisha timu ndogo ambazo mwanzoni hazikupewa nafasi, kama ambavyo Mashujaa ilivyowaondoa Simba kwa mara nyingine.

Hii isibakie kwa baadhi ya timu, umefika wakati klabu zote zikajiimarisha kwa kusajili wachezaji wenye uwezo na kuandaa programu nzuri za mazoezi na kwa kufanya hivyo, hakuna kitu kitakachoshindikana, tutashuhudia bingwa mpya ambaye hakutarajiwa, lakini hii itakuwa ni kutokana na maandalizi sahihi.

Kupata matokeo mazuri ni matunda ya uwekezaji, kila timu inatakiwa kuwa na mfumo mzuri wa kiundeshaji ambao utawafanya wasajili vikosi imara na vitakavyotoa ushindani na kuacha kuwa wasindikizaji katika kila mashindano yanayofanyika hapa nchini.

Kushuka daraja kwa Mtibwa Sugar, iwe somo kwa timu mpya zilizopanda daraja, lakini pia kwa klabu nyingine ambazo zimekuwa zikifanya maandalizi yake kwa 'mfumo' wa mazoea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ligi Kuu Bara 2023/2024 ilikuwa na mastraika butu

**WAUNGWANA** lazima tulonge, Ligi Kuu 2023/2024 ilikuwa na mastraika butu, haijawahi kutokea huko nyuma.

Ni msimu tulioshuhudia wachezaji wa nafasi ya viungo washambuliaji wakichuana wenyewe kwa wenyewe kuwania ufungaji bora.

Kwa straika wa timu yoyote ile ni lazima awe anajifikiria mara mbili mbili kama anaitendea haki nafasi yake.

Viungo washambuliaji, Stephane Aziz Ki wa Yanga, na mwenzake Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC ndiyo walioonekana kufukuzana kufunga mabao, na walikuwa wanafunga kweli kweli, ambapo wale wasiojua nafasi katika mpira wa miguu, wangedhani ni mastraika.

Aziz Ki ndiye kinara aliyemaliza na mabao 21, Fei Toto akawa na pili akipachika magoli 19.

Wakati wakipigania kiatu cha dhahabu na kuifanya vita kuwa kali, hakukuonekana juhudi zozote za washambuliaji kufurukuta, zaidi ya mmoja tu kwa mbali, ambaye ni Waziri Junior wa KMC.

Huyu amemaliza ligi akiwa amefunga mabao 12, na kushika nafasi ya tatu na kuonyesha angalau alikuwa anajisukuma, ingawa hakuwa mshindani halisi.

Matokeo yake pambano liliisha kama wengi walivyotegemea, mshindi wa kwanza na wa pili katika ufungaji bora Ligi Kuu msimu huu, wote ni viungo washambuliaji.

Achana na hilo, walioshika nafasi ya nne pia ni viungo washambuliaji, Saido Ntibazonkiza wa Simba na Maxi Nzengeli wa Yanga ambao kila mmoja amepachika mabao 11.

Twende kwa walioshika nafasi ya tano, ni winga na kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Kipre Junior, kiungo Marouf Tchakei wa Ihefu, pamoja na kiungo mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahya, ambao wote wamefunga mabao tisa kila mmoja.

Hadi nafasi yupo kiungo ambaye ni Gibril Sillah wa Azam FC, akifunga na straika Samson Mpangula wa Prisons, wote wakifunga mabao manane.

Hapa utaona kutoka nafasi ya kwanza hadi ya sita ambapo kuna wafungaji 10 bora, mastraika ni wawili tu, Waziri na Mbangula, ila kwa bahati nzuri wote ni Watanzania.

Ukiangalia takwimu hizo zinakuonyesha hata timu kubwa kama Simba, Yanga na Azam FC, hazikuwa na mastrika bora msimu huu. Walizidiwa hata na KMC na Prisons.

Msimu uliopita straika, Fiston Mayele wa Yanga alifungana na kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido.

Huko nyuma zaidi tuliona mastraika kama kina Meddie Kagere, John Bocco, Amissi Tambwe wakitamba kwenye ufungaji bora, lakini kwa sasa inaonekana kinyume chake. Sisemi viungo washambuliaji wasifunge mabao, au ni dhambi, lakini nimeandika hili kuwashtua mastraika wanaocheza Ligi Kuu waamke, pia viongozi wa klabu wangalie sasa ni jinsi gani na kusaka washambuliaji wenye ubora wa hali ya juu kama kina Kagere, Tambwe, Mayele na wengine wanaofanana na hao.

Katika soka, kazi ya kwanza ya kiungo mshambuliaji ni kutoa pasi za mwisho kwa mastraika, 'asisti' ya pili ni kufunga, na kazi namba moja ya straika ni kufunga mabao tu.

Matokeo yake tunaona sasa viungo washambuliaji wanafanya kazi namba mbili, ambayo ilitakiwa kufanywa na mastraika.

Sina uhakika, lakini inawezekana kabisa viungo washambuliaji hao waliwatengenezea sana mastraika wakashindwa kufunga, na ingewezekana wangekuwa na mabao mengi kuliko hayo ambayo wenzao wanayo.

Kwa hili kuna cha kujifunza kuelekea msimu ujao, kwani mastraika wote wa Kibongo na kigeni wamefeli.

Kuna haja ya viongozi wa klabu wanaosajili kuangalia mastraika wapya vijana kutoka klabu mbalimbali na kuacha kuwatumia wale wale wa miaka 'nenda rudi' wanaomaliza wakiwa na mabao matano au sita ambayo yanaweza kufungwa na mabeki tu.

Wanaosajili mastraika kutoka nje ya nchi watafute wale ambao wako kwenye viwango vya juu kwa wakati huo, na si kusajili kutokana na historia yao ya nyuma. au wale ambao wamemaliza mikataba kwenye klabu zao na hawawahitaji tena.



Ofisa Programu na Sera wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Rogathe Loakaki (kulia), akizungumza wakati wa mkutano wa vijana kwa ajili ya kutoa maoni kwenye mchakato wa maandalizi ya Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa 2025-2050, ulioandaliwa na mtandao huo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: TGNP**

# Mwinyi ahimiza amani kwa ustawi wa taifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza umuhimu wa kutunza amani kwa maendeleo na ustawi bora wa watu na taifa.

Amesema amani na kuwaunganisha watu kuwa kitu kimoja ni chachu ya kujenga ustawi bora wa jamii na kukuza uchumi wa nchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipokutana na Sheikh Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Madhehebu ya Shia Tanzania 'TIC' Maulana Sheikh Hemed Jalala Mwakindenge na ujumbe alioongozana nao.

Dk. Mwinyi alisema maendeleo ya nchi hayaji eneo lenye vurugu au vita, yanaboreshwa kwenye utulivu, umoja, usalama na mshikamano wa watu, pia nia rahisi kuyafikia.

Alisema hata kama hakuna maelewano kwa asilimia zote, hakuna jamii isiyo na migogoro lakini isipitilize ikawa tishio kwa amani, walau sehemu kubwa ya jamii iwe na maelewano ndipo mafanikio yanapatikana.

Pia aliwashukuru viongozi wa dini wa madhehebu yote na wananchi wa kuendelea kuhubiri na kuiombea nchi amani na mshikamano. Aliendelea kumuomba Mwenyezi Mungu kuidumisha nchi kwenye amani na utulivu kwa mafanikio makubwa.

Kadhalika aliwashukuru viongozi hao wa dini wa madhehebu yote kwa kuendelea kuwaombea heri, amani na mafanikio makuwa viongozi na serikali ili kuendelea kukamilisha vyema mipango ya sekali kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Naye Sheikh Jalala alimpongeza Rais Mwinyi kwa kazi nzuri ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali ikiwemo mafanikio makubwa yaliyofikiwa kwenye huduma za jamii, ikiwemo maji safi, umeme, elimu na afya, halikadhalika miundombinu ya barabara na mawasiliano.

Msemaji wa Jumuia hiyo, Yasmin Aloo, alipongeza mafanikio makubwa ya maendeleo yaliyofikiwa na awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Jumuiya ya Waislamu wa Madhehebu ya Shia Tanzania TIC', ilisajiliwa tangu mwaka 1992.

## Mbaroni madai kumuua mtalaka wake kisa mali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Jafari Magesa (31), mkazi wa Milambo kwa tuhuma za kula njama za kumuua mtalaka wake, Gaudensia Shukuru (25), mkazi wa Malunga, anayedaiwa kuuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kisha kutelekezwa katika pori la hifadhi ya Mkweni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi Mwanandamizi (SACP) Janeth Magomi, alithibitisha tukio hilo juzi na kwamba lilitokea Mei 27, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi.

Alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji na Kata ya Mwendele Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na jeshi lilipata taarifa hizo kupitia kwa mwenyekiti wa kitongoji.

"Wanandoa hao walikuwa na kesi ya talaka baada ya kuachana kwa sababu wanazofahamu wao. Kesi yao ilipangwa kusikilizwa Mei 28, mwaka huu, lakini imeshindikana baada ya kutokea kwa mauaji hayo siku moja kabla, hivyo tumemkamata mtalaka wake kwa upelelezi zaidi," alisema SACP Magomi.

Magomi alisema mwili wa Shukuru ulikutwa umekatwa na kitu chenye nchi kali mbele ya shingo yake na katika eneo la tukio msitu wa Mkweni, walikuta viatu vya kike vyenye rangi nyeusi na upelelezi unaendelea kubaini wahusika wote ili kuwachukulia hatua za kisheria licha ya kwamba wanamshikilia aliyekuwa mumewe.

"Chanzo cha tukio hili tumebaini ni migogoro ya talaka kati ya Shukuru na aliyekuwa mumewe. Tukio likatokea siku moja kabla ya kesi yao kusikilizwa," alisema.

Aidha, Magomi aliwataka wakazi wa mkoa wa Shinyanga kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi tena kwa kufanya mauaji kwa kuwa katiba ya nchi na vitabu vya dini vinakemea suala hilo na kusihi wanaotaka kuachana, wafanye hivyo kwa wema na si kufikia hatua ya kuuana.

# Wakurugenzi waonywa usiri madai walimu

**Na James Mwanamyoto,** BUKOBA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, amesema madai ya walimu yanayotokana na uhamisho na likizo si siri. Kutokana na hali hiyo, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuweka wazi orodha ya wanaodai na utaratibu wa malipo ya madai hayo ili kuondoa dhana potofu ya uwapo wa upendeleo pindi yanapolipwa na serikali.

Dk. Msonde ametoa wito huo kwa wakurugenzi wote wa halmashauri nchini wakati wa vikao kazi vyake na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu waliopo katika halmashauri za wilaya ya Bukoba na manispaa ya Bukoba.

"Wakurugenzi madai ya walimu si siri, yawekeni wazi ili mwalimu ajione ni wa ngapi katika orodha ya malipo na anadai kiasi gani," alisisitiza.

Dk. Msonde aliwataka wakurugenzi wanapowalipa walimu kupitia fedha za serikali kuu au mapato ya ndani, waweke wazi kiasi kilichopo na kitawalipa walimu wangapi kwenye orodha ya wanaodai. Alisisitiza kuwa kila fedha inayopokelewa kwa ajili ya kulipa wanaodai, iwekwe wazi ni kiasi gani kimepokewa na kitawalipa walimu wangapi.

Sambamba na hilo, Dk. Msonde alizitaka halmashauri kutohamisha watumishi kama hakuna ulazima na hakuna pesa za kugharamia uhamisho wa watumishi ili kuondokana na madeni yanayoepukika.

"Hamisheni walimu iwapo kuna ulazima unaotokana na ujenzi wa shule mpya na kwakuwa shule mpya zinajengwa kutokana na mipango inayotekelezwa, hivyo fedha kwa ajili ya uhamisho wa walimu zinapaswa kuwa zilitengwa pia," alisema. Dk. Msonde alihitimisha siku ya pili ya ziara yake mkoani Kagera kwa kufanya vikao kazi na maofisa elimu, maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika halmashaurui za manispaa na wilaya Bukoba.

# Uzio kudhibiti wanyamapori wakali wapunguza migongano kwa asilimia 80

**Na Jenifer Gilla**

UJENZI wa uzio wa umeme katika eneo la mapitio ya wanyamapori ya Nyerere Selous-Udzungwa, Halmshauri ya Mji wa Ifakara, umeelezwa kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori kwa asilimia 80.

Katika shoroba hiyo pia kumepandwa miti ya asili 40,000 kati ya 100,000 iliyodhamiriwa lengo likiwa kuweka mazingira rafiki kwa wanyamapori ili wasishawishike kuingia kwenye makazi ya watu, kuboresha hifadhi na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Wanyamapori wa Halmashauri hiyo, Goodluck Mallya, alisema hayo juzi kwa waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliokuwa katika ziara ya kuona maendeleo ya shoroba hiyo.

Alisema kabla ya kuwapo kwa uzio huo, walikuwa wanapokea taarifa za tembo kuvamia makazi ya watu na kufanya uharibifu mara mbili hadi tatu kwa wiki lakini sasa inaweza kupita mwezi bila matukio hayo kuripotiwa hali inayoonyesha mafanikio makubwa.

Mallya alisema mipango iliyopo sasa ni kuweka mizinga ya nyuki unapoishia uzio huo kudhibiti wanyamapori kuingia kwenye makazi ya watu ili kuwalinda wanakijiji na uharibifu unaotokana na matukio hayo na wao waone faida ya uwapo wa rasilimali hiyo katika eneo lao.

Alisema kwa kushirikiana na Shirika la Reforest Africa chini ya ufadhili wa Mradi wa USAID-Tuhifadhi Maliasili wa miaka mitano unaolenga kuongoa shoroba saba kati ya 61 zilizoko nchini, wanahamasisha upandaji wa miti katika shoroba hiyo ili kuiboresha na mpaka sasa wameshapanda 40,000

Meneja wa Programu wa Reforest Afrika, Lasima Nzao, alisema kupitia Mradi wa Urejeleshaji Shoroba kupitia ufadhili wa USAID Tuhifadhi Maliasili, wanapanda miti ya asili kwa kuchanganya mbegu za aina mbili na wanaipanda katika shoroba hiyo kwa kushirikiana na wanavijiji.

Alisema shughuli hiiyo inakwenda sambamba na utoji elimu kwa wakazi wanaoishi eneo linalozunguka hifadhi hiyo vikiwamo vijiji vya Sole, Mang'ula A na Kanyenja kuhusu umuhimu wa kupanda miti na kuitunza iliyopo kwa manufaa yao na shughuli za utalii.

Mratibu wa Programu wa shirika la Associazione Mazingira, Felister Mwalongo, alisema kupitia mradi huo, wanatoa elimu ya uhifadhi wa mazingira katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ili wawe mstari wa mbele kuitunza kwa manufaa yao.

Pia alisema wanatoa elimu hiyo katika shule za msingi na kupitia mradi huo wamesahawafikia wanafunzi 300 na walimu 45 na kugawa miche ya miti 60,000 ndani ya miezi minne.

Mkuu wa Uhifadhi wa Hifadhi Milima ya Udzungwa, Theodora Aloyce, alisema uwapo wa shoroba hiyo ni muhimu kwa sababu unasaidia wanyama kwenda sehemu zingine na kuzaliana, hivyo kuepusha wanyama wa aina moja kuzaliana na kupunguza maambukizi ya magonjwa.

Shoroba hiyo yenye urefu wa kilomita 13 inapita katika vijiji vya Sole, Kanyeja na Mang'ula A na inaunganisha Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

# Wajasiriamali wakumbushwa kuthibitisha ubora bidhaa

**Na Joseph Mwendapole,**
MBEYA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeendelea kuwahimiza wajasiriamali nchini kujitokeza kwa wingi kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa itawawezesha kuhimili soko la ushindani ikiwemo kuuza bidhaa zao bila vikwazo kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Udhibiti Ubora Ofisi ya TBS Kanda ya Mbeya, Ernest Simon, wakati akizungumza na wajasiriamali waliohudhuria Maonesho ya Mbeya Expo 2024, jijini Mbeya ambayo yalimalizika juzi.

Alisema kwa kutambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza uchumi, kila mwaka serikali hutenga fedha kwa ajili ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure.

"Kwa hiyo tumewafuata kwenye maonesho haya ili kuwapa elimu hii kwa sababu wengi huko mitaani hawana uelewa huo na wanadhani kuthibitisha ubora wa bidhaa kuna gharama nyingi.

"Tunawapa elimu ili waweze kufahamu kwamba serikali hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali pale wanapoomba bidhaa zao wanazozizalisha zithibitishwe ubora," alisema.

Alisema TBS wako kwenye maonesho hayo pamoja na mambo mengine kuwapa elimu na kuwahimiza wachangamkie fursa hiyo muhimu kwao.

Ili wajasiriamali wathibitishiwe ubora wa bidhaa zao, alisema wanatakiwa kuwa na barua ya utambulisho kutoka SIDO na baada ya kuipeleka TBS mchakato wa kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo unaanza.

Alisema uthibitishaji ubora wa bidhaa unamwezesha mzalishaji kupeleka bidhaa yake kwenye soko kwa kujiamini, kwani anakuwa na uhakika wa soko na bidhaa zake kushindana na za wazalishaji wengine kutoka ndani na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pia, alisema kuthibitisha ubora wa bidhaa kunamhakikishia mzalishaji kuwa bidhaa anayotaka kununua ni salama kwa afya yake.

Aidha, alisema uthibitisha bidhaa unamwezesha mzalishaji kupanua soko la bidhaa zake kwani Tanzania imeingilia makubaliano na nchi wanachama wa EAC kwenye mambo ya ubora na bidhaa ikishathibitishwa na TBS haitakiwi kupimwa tena na mashirika ya viwango ya nchi za jumuiya hiyo.

Aidha, Simon alisema kupitia maonesho hayo walitumia fursa hiyo kuelimisha wazalishaji na wananchi kwa ujumla majukumu ya TBS kuhusu udhibiti wa ubora wa bidhaa.

Pia aliwataka wafanyabiashara kusajili majengo ya biashara yakiwemo ya vipodozi, kwani hilo ni moja ya takwa la Sheria ya Viwango.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Jimbo la Kavuu, Geophrey Pinda (wa pili kulia), akipata maelezo alipotembelea eneo ilipotokea ajali ya Mtumbwi na kusababisha vifo vya watu saba, katika kijiji cha Ukingwamizi, kitongoji cha Itumba, mkoani Katavi juzi. **PICHA: WANMM**

# Pinda awafariji ndugu wa waliofariki ajali mtumbwi

**Na Munir Shemweta,**
MLELE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewatembelea na kuwafariji wananchi wa kijiji cha Ukingwamizi katika kitongoji cha Itumba kata ya Mwamapuri kutokana na watu saba kupoteza maisha kwa ajali ya mtumbwi.

Ajali hiyo ilitokea mwishoni mwa wiki iliyopita kutokana na maji kutoka mto Kavuu kuzunguka maeneo ya kitongoji cha Itumba na miili ya watu watano iliopolewa huku miili ya watu wawili ikiwa haijapatikana.

Akizungumza na wananchi wa kijiji Ukingwamizi juzi, Pinda amewapa pole wafiwa na kuwaeleza kuwa serikali iko pamoja nao katika kipindi hiki kigumu cha msiba wa ndugu zao waliopoteza maisha kwenye ajali.

"Serikali iko na nyie ndiyo maana mmeona walikuja na kulala hapa kuhakikisha wanafanikisha upatikanaji wa miili ya ndugu zetu," alisema Pinda

Aliwaomba wananchi wa kitongoji cha Itumba kuwa baada ya ajali hiyo, ni vyema wakaanza kuchukua tahadhari madhubuti kwa kuhakikisha vyombo vya usafiri wanavyotumia kwenye maji vinaimarishwa na kuangaliwa kila wakati kwa kuwa vikikaa muda mrefu vinaoza, hivyo kuwa rahisi kupitisha maji.

Pia ALIWATAKA wanaotumia mitumbwi kuhakikisha pia mizigo inawekwa kulingana na uwezo wa chombo sambamba na abiria wanaopanda kutokuwa wengi kupita kiasi.

Pinda aliwaeleza wananchi wa kitongoji cha Itumba kuwa kuna haja kwa sasa kuhakikisha mito kwenye halmashauri ya Mpimbwe inalindwa kwa kupanda miti katika kingo ili kuepuka uharibifu wa mazingira sambamba na vyanzo vya maji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpimbwe katika wilaya ya Mlele, mkoani Katavi, Shamimu Daud, aliwapa pole wananchi wa kitongoji cha Itumba kutokana na watu saba kupoteza maisha kwa ajali ya mtumbwi.

Alitoa shukurani za dhati kwa wananchi wa Itumba kwa kusaidia juhudi za kutafuta miili ya watu waliopoteza maisha katika ajali hiyo.

"Kwanza natoa shukurani za dhati kwa wale wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika eneo hili, wananchi ambao pia wamejitolea kuingia na kutafuta wenzetu na watumishi wote kwa kazi zilizofanyika hapa," alisema.



# Watumishi 5,000 wapandishwa vyeo miaka 3 ya Rais Samia

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATUMISHI 5,000 wa Mkoa wa Singida wamepandishwa vyeo na wengine 2,500 wameajiriwa katika kipindi cha miaka mitatu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema hayo jana kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa kwa ajili ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk.Emmanuel Nchimbi, ambaye yupo kwenye ziara ya siku tatu mkoani hapa.

Alisema katika kipindi hicho madeni ya watumishi Sh.bilioni 3.1 yamelipwa na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vijana, wanawake na walemavu imetolewa ya Sh.bilioni tatu

Dendego alisema katika kuwainua wananchi kiuchumi, kaya maskini 58,000 zimepewa Sh.bilioni 22 na kwamba Sh.bilioni 2.2 zipo benki zitaanza kukopeshwa vijana, wanawake na walemavu.

Aidha, alimhakikishia Katibu Mkuu wa CCM kwamba Serikali ya Mkoa huo itaendelea kusimamia kikamilifu fedha ambazo wanapatiwa na Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili wananchi waweze kupata huduma bora na za uhakika za maendeleo karibu na maeneo yao.

Dendego alisema mpaka sasa Mkoa wa Singida tayari umepokea zaidi ya Sh. trilioni 1.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hali ambayo imeufanya Mkoa wa Singida kung'aa kimaendeleo katika sekta mbalimbali.

Aliongeza kuwa Mkoa wa Singida kwa sasa unaendelea na mipango na mikakati ya kuwavutia wawekezaji katika sekta mbalimbali wa ndani na nje kuja kuwekeza mkoani humo, ikiwa ni sehemu ya kuongeza pato la mkoa na la taifa kwa ujumla kupitia vivutio vya uwekezaji kwenye masuala mbalimbali ikiwemo kilimo na utalii.

Naye Katibu Mkuu CCM, Dk.Nchimbi aliipongeza Serikali ya Mkoa wa Singida kwa kusimamia na kutekeleza kikamilifu ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi kwa kiwango cha juu ikiwemo miradi ya maji, afya, elimu na miundombinu mkoani humo.

Dk. Nchimbi alisema ushirikiano imara kati ya viongozi wa serikali na wa CCM mkoani Singida umesababisha miradi mingi ya maendeleo kutekelezwa kwa wakati na kwa kiwango cha juu.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mkufunzi wa Chuo cha VETA Dodoma, Yusufu Haule (kulia), alipotembelea banda la maonyesho la VETA Dodoma katika Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu katika viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga jana. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian. **PICHA: OWM**

# Dodoma, Tabora vinara matukio ya ukatili wa kijinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KESI za ukatili wa kijinsia zaidi ya 300 ikiwemo mimba na ndoa za utotoni pamoja na manyanyaso kwa watoto wa kike zimeripotiwa, huku Mkoa wa Dodoma na Tabora ikionekana kuwa kinara wa matukio hayo.

Kutokana na hali hiyo wadau wa masuala ya kupinga ukatili wameliomba Bunge kuiboresha Sheria ya Ukatili ili iwe na makali ya kuwawajibisha watu wanaohusika na vitendo hivyo.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Msichana Innitiative, Rebecca Gyumi, alisema hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano wa masuala ya ukatili kwa mtoto wakike.

Alisema kesi za aina hiyo zimekuwa zikicheleweshwa mahakamani kutokana na baadhi ya wahusika kutoa fedha kwa ndugu wa mtoto aliyebainikwa kupata manyanyaso. Alisema wamekuwa wakikutana kila mara katika majukwaa mbalimbali ya kupinga ukatili wa kijinsia na hilo limekuwa likipewa kipaumbele, hivyo serikali ijitahidi kuiangalia sheria ya makosa hayo ili waifanyie kazi. Alisema katika utekelezaji wa kupinga masuala ya unyanyasaji kwenye mikoa minne ambayo wanatekeleza, tatizo la ukatili limeonekana kuwa sugu na linahitaji kufanyiwa kazi.

"Tunaendelea kupiga vita suala la ukatili wa kijinsia kwa watoto, tunahitaji sapoti kutoka kwa jamii ili kutokomeza suala hilo,"alisema Gyumi.

Alisema katika mkutano huo washiriki kutoka kata 44 wamehudhuria lengo ni kuhakikisha wanatokomeza masuala ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Lucia Nzige alisema jamii imekuwa ikiamini kuwa mtoto wa kike siyo wa kupata elimu, badala yake anapaswa kuolewa.

## Mashekhe wapewa jukumu kudhibiti mmomonyoko maadili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limewataka mashekhe wa kata kudhibiti mmomonyoko wa maadili, ili jamii iweze kudumisha misingi ya dini na waumini wazingatie kanuni na sheria wanazofundishwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wakidhibiti mmomonyoko huo kutasaidia kuendeleza nidhamu na heshima ndani ya jamii na kuwezesha kutoa mazingira bora ya malezi kwa watoto na vijana, ili na wao waweze kufanya ibada kwa unyenyekevu na kuimarisha mahusiano yao na Mungu.

Pia, aliwataka mashekhe hao kudhibiti migogoro na mizozo inayojitokeza ndani ya miskiti, ili kuzuia vitendo vya udanganyifu, ulaghai inayoweza kujitokeza kutokana na ukosefu kwa maadili ya kiroho.

Kadhalika, alitoa onyo kwa kuwataka mashehe ambao hawatakuwa na kasi kwenye utendaji wao ni vizuri wakaachia nafasi hizo badala ya kuendeea kunga'ng'ania na kuukwamisha uislamu.

Alisema BAKWATA wilaya kupitia mwongozo uliotolewa na Mufti Mkuu wa Tanzania kamwe hautakuwa tayari kufanya kazi na viongozi wanaofanya kwa mazoea kwenye nafasi zao.

## Mahakama Singida yatupa shauri la rufaa ya talaka

**Na Elisante John,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Singida, imetupilia mbali shauri la rufaa ya talaka, iliyowasilishwa na Swalehe Sengi (33), dhidi ya Fatuma Juma (29), baada ya kubaini mkata rufaa alikuwa na nia ya kumdhulumu mtalaka wake ngalawa 30 za kuvulia samaki na nyumba moja.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Singida, Fadhili Luvinga, alisema ameridhishwa na hukumu iliyotolewa awali na Mahakama ya Mwanzo, Sepuka na kwamba, nyumba inayolalamikiwa na mkata rufaa ni halali kwa mtalaka wake (aliyekuwa mkewe), kutokana na ushahidi uliowasilishwa mahakamani.

Alisema baada ya kupitia ushahidi katika nakala ya rufaa, mahakama imejiridhisha wala pasipo kuacha shaka yoyote kuwa nyumba anayoidai mrufani, imetokana na juhudi na uwekezaji wa mwanamke na siyo ya mwanaume, hivyo uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Mwanzo Sepuka, unabakia kama ulivyo.

Kadhalika kuhusu mgawanyo wa ngalawa 30 za kuvulia samaki ambazo mwanaume (mrufani) aliiomba mahakama iamuru apatiwe zote, Luvinga alipinga hoja hiyo na kuagiza zigawanywe nunu kwa nusu, yaani kila mmoja apatiwe 15, ili kila mmoja aendelee na shughuli za uzalishaji mali, kama ilivyoamuriwa na Mahakama ya Mwanzo Sepuka.



# Matukio ya mauaji Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma amesema matukio ya mauaji yamekuwa yakiongezeka visiwani Zanzibar.

Amesema kwa mwaka 2023 jumla ya matukio 44 yameripotiwa ukilinganisha na matukio 33 yaliyoripotiwa mwaka 2022.

Aliyasema hayo jana katika Baraza la Wawakilishi Chukwani, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir aliyetaka kujua takwimu za makosa mbalimbali ikiwemo ya jinai yaliyoripotiwa Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Hamza alisema serikali imeanza kufanya utafiti wa kina kutaka kujua sababu za kuongezeka kwa matukio ya mauaji zaidi ukilinganisha na udogo wa idadi ya wananchi wa Zanzibar.

Alisema katika hatua za awali imebainika matukio hayo yanasababishwa na vijana wanaojishughulisha na matumizi ya dawa za kulevya na kuwashambulia wananchi kwa kutaka kuwapora vitu vya thamani.

Hamza alisema baadhi ya matukio yamekuwa yakifanyika mchana na mengine usiku ambapo vijana huvamia nyumba za wananchi na kufanya matukio ya uhalifu ambayo hutishia uvunjifu wa amani.

Alizitaja juhudi zinazochukuliwa kwa sasa katika kukabiliana na matukio hayo ni pamoja na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha operesheni ya kusaka makundi ya vijana ambao wanatumia silaha za jadi ikiwemo mapanga na nondo.

Alisema tayari operesheni hiyo imeanza kwa upande wa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kufanikiwa kuwanasa zaidi ya vijana 250 wakituhumiwa kujishughulisha na matukio ya uhalifu.

Aliyataja maeneo ambayo yanaongoza kwa matukio ya uhalifu kwa vijana kutumia silaha za jadi ni Mboriborini, Kinuni, Bububu na Miembeni ambayo yote vijana hujishughulisha na matumizi ya dawa za kulevya.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita akizungumza wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Hewa ya ukaa chanzo mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman amesema hewa ya ukaa ni miongoni mwa gesi chafu zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi, yanayotokana na ongezeko la joto duniani.

Alisema gesi chafu hizo ambazo kwa pamoja zinaitwa 'gesijoto' zinatokana na shughuli mbalimbali za binadamu ambazo huzagaa kwenye usawa wa dunia na kusababisha kuongeza kwa joto duniani. Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua tathmini ya hewa ya ukaa ipoje kwa mustakbali mzima wa mabadiliko ya tabianchi.

Waziri huyo alisema hewa ukaa huchangia kwa zaidi ya asilimia 70 ya gesijoto duniani na kipimo cha gesi joto hupimwa kwa kiwango cha hewa ukaa.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2012 ni kuwa kiwango cha uzalishaji wa hewa ukaa na gesijoto Zanzibar ni kidogo sana ambacho ni wastani wa tani 0.6 ya hewa ukaa kwa mtu.

Alisema kiwango hicho kinategemewa kupanda ifikapo mwaka 2030 na kufikia wastani wa tani 1.02 ya hewa ukaa kwa mtu, kwamba pamoja na kiwango hicho lakini bado kidogo sana kulinganishwa viwango viliopo vya kikanda na duniani.

"Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Zanzibar siyo mchangiaji wa mabadiliko ya tabianchi na athari zake zinazoikumba dunia hivi sasa kwa kuwa inazalishaji kiwango kidogo sana cha gesijoto zinazosababishwa mabadiliko hayo" alisema.

Hata hivyo, alisema Zanzibar imekuwa ikiathiriwa na mabadiliko hayo katika nyanja za kimazingira, kijamii na kiuchumi.

# Serikali, sekta binafsi kutafuta soko la vanila

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema inatambua uwepo wa changamoto ya soko la vanila kwa wakulima.

Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis alisema kufuatia hali hiyo wanachukua hatua za kushirikiana na sekta binafsi kutafuta soko la zao hilo ili kuongeza faida zaidi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mtabwe, Dk. Muhammed Ali Suleiaman aliyetaka kujua Je?, Serikali inalitambua tatizo hilo la soko kwa wakulima wa vanila, na ni hatua gani inazichukua katika kuwasaidia wakulima kukabiliana na changamoto za soko.

Akijibu swali hilo, Waziri Shamata alisema kwa sasa, serikali inashirikiana na kampuni mbili za wanunuzi, kampuni ya Blue Spice na kampuni ya Zenji Spice, ambazo zinanunua vanila kwa kiasi kikubwa na kusafirisha nje ya nchi.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2021-2023, takwimu za uzalishaji wa zao la vanila tani 86.18, hiliki tani 1.06, mdalasini tani 42.9, pilipili manga tani 27.25 na kungumanga tani 26.75.

Alisema: "Mheshimiwa Spika, serikali inaendelea kushirikiana na mashirika binafsi pamoja na wawekezaji wa sekta ya kilimo ili kuongeza ubora na thamani ya bidhaa za viungo ili kuyafikia masoko mengine zaidi ikiwemo soko la utali".

# Shule 217 kuunganishwa na mkongo wa taifa

**Na Gwamaka Alipipi**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema katika kutekeleza mageuzi makubwa ya elimu kidigitali shule 217 zinatarajiwa kuunganishwa na mkongo wa taifa kwa ajili ya kupata mawasiliano ya kisasa ya teknolojia ya TEHAMA.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa jMwanakwerekwe Ameir Abdalla Ameir, aliyetaka kujua hatua zilizofikiwa kwa sasa katika mageuzi makubwa ya elimu ya mtandao.

Gulam alisema jumla ya shule za sekondari 217 zinatarajiwa kuunganishwa na mkongo wa taifa wakati vituo vya ubunifu Hub 22 vitapata huduma za mawasiliano ya mtandao.

Aidha, alisema vituo vya mafunzo kwa walimu 10 vinatarajiwa kuunganishwa na huduma za mtandao na kasi wa mawasiliano kwa ajili ya kuwawezesha walimu kutekeleza majukumu yao.

Alisema shule zote ziliopo katika visiwa vidogo zitaunganishwa na huduma za mawasiliano ya huduma za Intaneti kupitia mkongo wa taifa.






Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 1, 2024




# KAACHWA MWINGINE wanaume sasa wanasutana

HATIMAYE ndoa iliyokuwa ikitikisa kwa mastaa wa Bongo kati ya Shilole na Rommy imefikia ukingoni, na kuibua hisia tofauti kwa Watanzania.

Shilole ambaye licha ya kupata umaarufu kupitia tasnia ya sanaa ya filamu na muziki, amesifika kwa kuwa na uhusiano tofauti na wanaume wenye umri mdogo kuliko yeye.

Kibaya zaidi, kila mwanaume aliyeishi naye ukianzia kwa Nuh Mziwanda, Uchebe na sasa Rommy, anapoachwa kunaibuka maneno mengi yanayoleta taharuki.

Awali kulikuwa na uvumi kuwa ndoa ya Shilole na Rommy ambaye alikuwa mpiga picha wake imefikia mwisho, kabla wenyewe kujitokeza hivi karibuni na kuthibitisha jambo hilo.

Baada ya Rommy kutoa tangazo kuwa ni kweli yeye na Shilole wameachana na kueleza anamuachia kijana mwenzake andeleze gurudumu, mume wa zamani wa Shilole, Uchebe alijitokeza na kuanza kumnanga mwenzake na kudai anataka huruma kutoka kwa watu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Uchebe ametoa mfululizo video na ujumbe wa kumponda Rommy kuwa aache kulia kwani maisha hayo aliyapitia miaka 10 iliyopita na sasa ameyasahau.

"Mimi sikai kwa mwanamke, unapiga kelele kwa ajili ya mwanamke, maisha hayo nimeyasahau miaka 10 iliyopita," amesikika akisema katika moja ya video yake.

Hata hivyo, Rommy ameonekana kuwa mtulivu na sakata hilo, na badala yake amekuwa kimya bila kujibu chochote kutokana na kauli za Uchebe.

BASI SAWA

## Mwijaku imekuaje hapo?



MSANII maarufu wa filamu na mtangazaji, Mwijaku, hatimaye amejiunga katika redio inayomilikiwa na mwanamuziki Ali Kiba.

Katika ujumbe wa Ali Kiba katika ukurasa wake wa Instagram, amempongeza Mwijaku kwa kujiunga naye na kumtaja kama mtu ambaye alimfikiria wakati akianzisha chombo hicho.

Hata hivyo, Mwijaku amesema amekwenda katika kituo hicho baada ya kupewa malipo makubwa na ahadi ya kulipiwa masomo ya juu ngazi ya shahada ya uzamivu.

## Willy Paul amtaja Brown



MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Willy Paul, amesema mipango yake ndani ya miaka miwili ni kufanya kazi na msanii maarufu wa Marekani, Chriss Brown.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Willy Paul amesema nafasi aliyokuwepo sasa inafaa kufanya kolabo na wanamuziki wakubwa wa Afrika na Marekani.

Amewataja wasanii ambao ana mipango nao kuwa ni Chris Brown kutoka Marekani na Burna Boy wa Nigeria.



## HAMISA MOBETTO AMEJIBU...

BAADA ya kuhusishwa kuwa yuko katika mahaba mazito na mwanasoka Aziz Ki, mrembo Hamisa Mobetto, ameamua kutoa majibu ya mbali na kwaambia wanaoumia na suala hilo watambue kuwa ni bahati yake.

Bila kueleza kama hilo ni jibu kwa kile kinachoendelea mitandaoni kuhusu penzi lake jipya, Hamissa ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram, kwamba kila bahati inakuja na jitihada.

"Kuna wakati bahati ni bora kuliko juhudi, ila bahati inakuja baada ya jitihada na juhudi," ameandika mrembo huyo.



## Harmonize ameanza kutulia

MKALI wa muziki wa Bongo Fleva, Rajab Kahali, maarufu kama Harmonize, amejivunia kuwa na bahati kuwa baba wa mtoto ambaye ni mwanamke.

Katika ujumbe wake kwa binti yake Zuuh Konde, amesema amebahatika kuwa baba wa binti huyo na kwamba atasimama imara kuhakikisha anamuongoza katika maadili na maelekezo mazuri.

Harmonize amekuwa mfano kwa wasanii maarufu kwa mtoto wake kutomuangazia mara kwa mara katika mitandao ya kijamii na hufanya hivyo inapotokea jambo la muhimu pekee.

## MAMBO NI KOMASAVAA, DISCONECT

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Mei ulioisha jana ulikuwa na hekaheka kubwa kwenye eneo la muziki, hasa wa bongo fleva.

Wasanii wakubwa nchini kama Diamond Platnumz, na mwezake Harmonize, walikuwa bize, na wakatoa ngoma ambazo zimeonekana kubamba kweli kweli, si kwa mashabiki wao tu, bali hata kwa muziki huo kwa ujumla.

Mbali na wasanii hao, wasanii mbalimbali hawakuwa nyuma kutoa pini ambazo zimeonekana kukonga mioyo ya mashabiki wa muziki kwenye sherehe, madisco, mitaani, redio na televisheni, hadi mitandao ya kijamii. Kwa ujumla Mei ni mwezi ambao haikupoa. Hebu tuangalia ngoma kali zilizotolewa mwezi huo, na kwa sasa ndizo habari ya mjini.

**Komasava-Diamond Platnumz**

Picha linaanza tu, Mei 3, msanii kinara wa muziki wa kizazi kipya nchini, Diamond Platnumz, alidhihirisha ukinara wake, alipokuwa wa kwanza mwezi huo kupandisha ngoma yake aliyowashirikisha, Khalil Harisson na Chley, akaiita, 'Komasava.' Mpangilio wa muziki huo, uvaaji na uchezaji, umekuwa gumzo kubwa kwenye mitandao ya kijamii.

**Nibusu-Barnaba ft Yammi**

Shughuli iliendelea, Mei 8, ambapo msanii mkongwe, Barnaba alipofyatua ngoma yake aliyoiita,'Nibusu', akamshirikisha mwanadada, Yammi. Hapo sasa mwezi ukaanza kuchangamka, kwani ngoma hiyo ilipata mashabiki wengi na hadi leo imeonekana kuangaliwa sana kwenye mtandao wa,'youtube.'

**Disconnect-Harmonize ft Marioo**


Siku tisa baadaye, Mei 17, Tembo, Harmonize, akatimba na ngoma yake iliyopewa juna la 'Disconnect' ambayo na yeye hakuwa pele yake, akamshirikisha Marioo. Mambo yakawa moto kweli kweli, mashabiki wakaanza kutafutana.

**Kunguru-Mbosso**

Siku hiyo hiyo, wakati Harmonize alitambulisha ngoma yake Mei 17, upande wa pili, Mbosso alipandisha ngoma yake, akaiita 'Kunguru Challenge.' Ngoma hiyo imetokea kupendwa sana kutokana kuwa na maneno ya kiswazi mno. Video yake ndiyo imewavunja watu mbavu, kutokana msanii huyo, kuigiza kama m'dada fulani hivi.

**Lonely-Yammi ft Nandy**

Nani alisema eti wanawake hawapendani? Mei 22, msanii Yammi, alitambulisha ngoma yake iitwayo, 'Lobely.' Mwenyewe alikaa, akaona hii ni lazima amshirikishe shosti, Nandy. Ni ngoma ambayo ni gumzo hivi sasa.



FILAMU

## Shemeji mtata, ka' viazi mbatata




**Na Adam Fungamwango**

KUNA mambo mengine yanashangaza sana. Yaani mtu anatoka nyumbani kwake kwenda kuishi kwa mtu mwingine, kwa sababu tu ya kufikiria kule kuna malisho mazuri kuliko kwake.

Kuna hii filamu ya 'Utata wa Shemeji' inayoonyesha jinsi baadhi ya watu ambao wanafikiri kuwa mjini ni kila kitu. Yaani mtu akisikia Dar es Salaam, basi anaona kama vile ni sehemu ya raha tu.

Kila kitu atakipata bure. Au maisha yake ni rahisi sana. Ukweli sivyo hivo. Dar es Salaam ni jiji lenye changamoto nyingi. Kila kitu ni pesa.

Barton anachoka maisha ya shamba. Anaona kwake ni magumu licha ya kwamba ana nyumba na shamba. Anachofanya ni kuuza shamba na nyumba kijijini na akili yake ikamtuma kwenda mjini Dar es Salaam kwa dada yake.

Dada yake ameolewa jijini Dar na mwaume ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa fulani. Anafika Dar na kupokewa, lakini hasemi kama atarudi lini.

Kinachofanyika kwake ni kwamba akapewa lifti, lakini akataka kupiga na honi. Barton akawapanda kichwani dada yake na shemeji ya Kalawi.

Kalawi kila akimuuliza mkewe kaka yake ataondoka lini kwa sababu mambo ya mjini wamepanga chumba kimoja na sebule, kaka analala sebuleni si vizuri.

Kibaya zaidi ni kwamba Barton alikuwa hataki kufanya kazi yoyote ile, bali kukaa nyumbani tu.


Mke anaona kama vile mumewe ana roho mbaya hataki ndugu wawepo. Baada ya kuzoea shemeji sasa nyuma ikawa kama ya kwake.

Akakutana na wanawake wa mjini. Akawa anawaleta hadi nyumbani kwa shemeji yake. Kibaya zaidi akawa anawadanganya kuwa nyumba ile ni ya kwake.

Akawa kama yeye ndiyo baba mwenye nyumba na wenzake ndiyo wamewekwa tu hapo.

Mwisho wa siku, baada ya shangingi lake kupata taarifa sahihi kuwa nyumba ile si ya kwake ni ya shemeji yake na amepanga, mwanamama huyo akaamua kuvunja uhusiano.

Mwisho akaomba msamaha na nauli arudi kijijini. Shemeji na dada yake wakamsamehe, wakampa nauli, na pesa za kununulia shamba lingine ili aanze tena maisha mapya huko kijijini.



# Ayra 'kitete' cha nini?

MWANAMUZIKI wa Afrobeats Ayra Starr, amesema alipokutana na msanii maarufu wa Marekani, Rihanna, alijikuta na furaha iliyopitiliza na kushindwa kumwambia kitu chochote.

Katika mahojiano na Beat FM, mwimbaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alikutana na Rihanna kwenye Tukio la Authentic Woman huko London mapema mwezi huu, alijikuta akiwa na 'kitete' ambacho alishindwa kufanya jambo lolote.

"Jambo la kuchekesha ni kwamba kabla sijakutana na Rihanna nilitamani kuzungumza naye kama rafiki, ninahisi kama angependa muziki wangu. Lakini nilipokutana naye nilichanganyikiwa ajabu, nilishindwa kuongea," amesema Ayra.



## Diddy kukosa siku adimu ya binti yake

RAPA mkongwe nchini Marekani, P Didd, atashindwa kuhudhuria sherehe ya kuhitimu kwa binti yake kutokana na kukabiliwa na kesi kadhaa za unyanyasaji wa kingono.

Diddy anakosa baadhi ya matukio muhimu kwa watoto Binti yake Chance mwenye umri wa miaka 17, anatarajiwa kuhitimu katika shule ya Sierra Canyon katika eneo la Los Angeless, lakini baba yake atashindwa kuhudhuria kutokana na kuwa na matatizo ya kisheria.

Imeelezwa Didd tayari aliwasilisha taarifa ya kutohudhuria katika sherehe hiyo, badala yake wanafamilia wengine watakwenda kumwakilisha.


## Ara umeushinda mfumo dume

MPIGA ngoma maarufu kutoka Nigeria, Araola Olamuyiwa, anayejulikana kama Ara, amesema aliwahi kuambiwa na wanaume kuwa hawezi kupata watoto iwapo atapiga kifaa hicho.

Akiongea hivi karibuni, Ara alikumbuka jinsi alivyohangaika kupata mtu wa kumfunza kucheza ngoma baada ya wanaume kumkatalia.

Ara alieleza kuwa kwa sababu jamii ya wapiga ngoma walikuwa wametawaliwa sana na wanaume, iliwashangaza kuona mwanamke akitaka kujifunza ufundi huo na kuwa macho.





## Johnny Wactor afariki dunia

MWIGIZAJI maarufu katika uigizaji, Johnny Wactor, ambaye anajulikana kama Brando katika filamu ya General Hospital, amefariki dunia katika tukio la kupigwa risasi.

Muigizaji huyo aliuawa si wakati wa tukio la jaribio la wizi katika jiji la Los Angeles, Mei 26, mwaka huu.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Wactor (37), alikuwa akijaribu kuzuia wizi wa fedha baada ya kuibuka mzozo uliogeuka kuwa majibizano ya risasi.

## Young: kila zuri halikosi chungu

MWIMBAJI na mtayarishaji wa muziki nchini Nigeria Young John, amesimulia jinsi alivyofukuzwa mbele ya kamera wakati wa upigaji picha wa video ya wimbo ambao alioshirikishwa.

Katika mahojiano na MTV Base Africa hivi karibuni, msanii huyo alielezea mwanzo wake katika lebo ya rekodi ya YBNL, amesema aliondolewa kuchukuliwa picha katika wimbo wa Awoon Goons Mi wa mwanamuziki maarufu Olamide.

"Hakuna anayependa kusema matukio yake ya uchungu, miaka kadhaa iliyopita katika wimbo wa Olamide ulitayarishwa na Pheelz na mimi, lakini nilifukuzwa wakati tukichukua picha ya video, nilipata uchungu sana," amesema





# BoT yaeleza faida matumizi kidijitali huduma za fedha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Yamungu Kayandabila amesema matumizi ya kidijitali katika utoaji wa huduma za fedha inasaidia kuchangia maendeleo endelevu katika soko la kifedha pamoja na utoaji taarifa sahihi na kwa wakati.

Aliyasema hayo juzi jijini Arusha wakati akifungua semina ya siku tatu iliyoandaliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), kwa kushirikiana na BoT.

Alisema ubunifu wa mabadiliko ya kidijitali utarahisisha taarifa za kifedha kupatikana kwa wakati na kwa uwazi zaidi.

"Faida za mabadiliko ya kidijitali ni uwezo wa kutoa huduma za kifedha ambazo hazijafikiwa kuendesha ushirikishwaji wa fedha kwa kupanua benki ya simu na nyingine za kidijitali na bidhaa zinazostawi,"alisema.

Alisema ujio wa mabadiliko ya kidijitali kunahitajika uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya teknolojia, uboreshaji endelevu wa nguvu kazi na hatua za usalama wa mtandao.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA,Pius Maneno alisema mkutano huo umeshirikisha washiriki zaidi ya 700 kutoka sekta za umma na binafsi nchini.

Alisema wamejadiliana mada ndogo 11 ambazo zitalenga kuangalia wakaguzi wa ndani kuhusu masuala ya kidijitali pamoja na kuangalia miongozo mbalimbali iliyopo.

Pia, alisema mada nyingine itahusisha maendeleo endelevu kwa kutumia dijitali katika masoko ya hisa ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, changamoto za matumizi ya kidijitali, masuala uwekezaji endelevu na utoaji wa taarifa.

# 'Wazalishaji vyakula vya wanyama zingatieni ubora'

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imewataka wazalishaji na wasambazaji wa rasilimali na vyakula vya wanyama kuhakikisha vyakula na viwanda vyao vimekaguliwa na kufikia ubora wa usalama unaohitajika.

Wito huo umetolewa juzi jijini Arusha wakati wa kuhitimishwa kwa ziara ya kikazi ya siku tatu ya wakaguzi wa vyakula vya mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA).

Mkurugenzi wa Huduma za Uchunguzi kutoka TVLA, Dk. Zacharia Makondo, alisema ni muhimu kwa vyakula vya mifugo kufika sokoni kama vilivyowekwa viwandani na kwamba wanaopuuza suala la kupima na kuhuisha usajili wa viwanda vyao watachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama.

Alisema kuwa katika utekelezaji huo ambao hawajasajiliwa watawafungia na hawataruhusiwa kufanya shughuli zao, huku akibainisha kuwa maabara za kanda zitawezeshwa kuwa na vifaa vya kufanya ukaguzi katika maeneo ambayo yanauhitaji mkubwa wa kufanywa kwa ukaguzi wa rasilimali za vyakula na vyakula vya mifugo ili kuhakikisha vinakuwa salama.

Mtaalamu wa Mifugo, Idara ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Theodata Sallema, alisema wakaguzi wanapaswa kufanya ukaguzi katika maeneo yao na kuhakikisha wadau wanafuata sheria.

Alisema wanaofunga vyakula vya mifugo au madini katika vifungashio vidogo wahakikishe vinakuwa na lebo na maelezo ambayo yanaendana na mfuko wa awali ambao wameufungua.

Pia, alisema wizara inaendelea kuwashukuru wadau kwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa na kwamba changamoto zilizobainishwa zitawasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Meneja wa TVLA Kanda ya Kaskazini – Kituo cha Arusha, Dk. Rowenya Mushi alisema kanda hiyo ambayo inahudumia mikoa mitatu ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro imepata chachu ya kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa wazalishaji na wasambazaji wa vyakula vya mifugo juu ya kupima vyakula vyao kuwa na ubora na kuleta matunda kwa wafugaji.

Pia, aliwasihi wazalishaji wa vyakula vya mifugo kufikisha sampuli ya vyakula vyao katika maabara ya TVLA katika kila toleo kuhakikiwa ubora na kupatiwa elimu na ushauri juu ya vyakula hivyo, ili kuleta tija kwa wafugaji wanaotegemea vyakula hivyo.




Mkazi wa Kilapula, kata ya Ngomeni, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Ramadhani Bakari Iddi (46) akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kuhukumiwa na Mahakama ya Wilaya hiyo mapema wiki hii, kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumlawiti mtoto wa miaka 13. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanafunzi 4,000 wanufaika na mradi wa STEM

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAFUNZI zaidi ya 4,000 wa shule za msingi saba katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wameanza kunufaika na mradi wa Sayansi Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), unaofadhiliwa na Marekani.

Ufadhili wa mradi huo umelenga kuwahamasisha wanafunzi wa kike na wa kiume kupenda kusoma masomo ya sayansi na kuwa wabunifu.

Akizungumzia mradi huo, Meneja Mkaazi wa Shirika la So They Can Tanzania, Roselyne Mariki, ambao ni watekelezaji wa mradi huo alisema mradi umetekelezwa kwa kipindi cha miezi minne.

Aidha, alisema wanafunzi walionufaika moja kwa moja ni 536, lakini wamejumuishwa na wa nje ambao hawakuwa wanufaika wa moja kwa moja na kufikia idadi ya wanafunzi zaidi ya 4,000.

Alisema mradi ulitambulishwa katika shule za msingi 31 za halmashauri hiyo, walipojadiliana na wataalamu wa elimu kutoka halmashauri pamoja na walimu waliamua mradi uanze kwa majaribio kwenye shule nne japokuwa umekwenda mpaka shule saba. Pia, alisema walimu waliowekwa kwenye mradi kwa kila shule hawapungui wanne la jumla yao ni zaidi ya walimu 30, ambao walipatiwa mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kusaidia kufundisha wanafunzi ubunifu.

Aidha, alisema kutokana na maboresho yaliyofanywa na serikali kwenye mtaala mpya wa elimu na sera wamejipanga kuanzia madarasa ya chini, ubunifu waliowapa wanafunzi hao utawasaidia kwenda na mabadiliko ya mtaala na sera na watakuwa na uweledi katika masomo ya sayansi hayo.

Alisema baada ya kuanzisha mradi huo, kumekuwapo na mwamko wa wanafunzi kupenda masomo ya sayansi, hivyo anaamini wataendelea, huku akiahidi kuendelea kuwawezesha kupitia mradi wao wa sauti yangu.

Mratibu wa STEM, kutoka Shirika la Projekt Inspire, Mashambo Kisakeni, alisema mradi huo wanafunzi waliwafundisha kwa vitendo, walilenga vipaji, ubunifu na ushirikiano.

Alisema walianza kuwanoa walimu ili wakawafundishe wanafunzi kitu ambacho alieleza kuwa kimewasaidia kwa kuwa wamekuwa wabunifu wakiwamo waliobuni fimbo nyeupe ya kutumia walemavu wasioona, gesi, ndege na kuirusha, waliojenga nyumba na vitu vingine vya asili.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Getrude Kavishe, alisema kuanzishwa kwa mradi huo kumewasaidia kupunguza utoro katika shule nyingi za msingi kwa kuwa wanafunzi walipenda kwenda kujifunza ubunifu wa vitu.

Aidha, alisema vifaa vingi walivyokuwa wanatumia ni zana za kufundishia ambazo ziko kwenye maeneo yao, hivyo walimu ni bora wawaelekeze wanafunzi namna ya kufanya ubunifu.

Pia, alisema katika mtaala mpya wa elimu wanakwenda kufanya kwa vitendo zaidi kuliko nadharia.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anna Mbogo, alifurahishwa na ubunifu aliouona kwa wanafunzi, huku akishuhudia vitu walivyobuni.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Uaminifu uliopitiliza zama zile, unadondosha barua na inafika

## -Unakwama kijijini, unalala,kula kwa mjumbe bila shida

**Na Adam Fungamwango**

KWA jinsi watu wa sasa walivyokosa uaminifu na teknolojia ingekuwa kama ile ya zamani sijui ingekuaje!

Yaani sipati hata picha. Hakuna miundombinu mizuri ya barabara, hakuna mawasiliano ya simu za mkononi kama hivi sasa, huduma za pesa kwenye mitandao, na hata mitandao ya kijamii ambayo inasababisha watu kuwasiliana popote pale na hata kutumiana pesa.

Mambo yote haya ya teknolojia yalianza katikati ya miaka ya 1990, lakini kurudi nyuma ilikuwa ni aina fulani ya maisha ambayo yalikuwa na changamoto nyingi, ingawa zimeonekana hivyo baada ya utawandazi kuja. Kipindi hicho watu waliona maisha ni sawa tu, hakuna tatizo lolote.

Ni kipindi ambacho mtu na mkewe, mumewe au mpenzi wake mmoja akisafiri hawatoonana wala kuongea tena mpaka arejee kwa muda wote ambao mmoja yupo safarini.

Labda tu, aandike barua na kuituma posta kumjulisha kuwa amefika. Na hiyo ni lazima anayetarajiwa kupokea barua awe ana sanduku la posta, la ofisini mwake, jirani au mtu anayemfahamu.

Ila tu lazima utambue kuwa itafika baada ya muda mrefu, ambao ni kuanzia wiki mbili na kuendelea.

Siku hizi siyo tu kwamba mke, mume au mpenzi wanaweza kuwasiliana muda wowote ule, hata mmoja akiwa nje ya nchi, lakini pia kuna 'video call', ambayo wanaweza kupigiana na wakaonana huku wakizungumza.

Ngoma nyingine ni pale ambapo mtu anamkatia tiketi mkewe kwenda kijijini kutazama wazazi wake, halafu hampi nauli ya kurudia.

Kipindi kile ilikuwa lazima anayesafiri kutoka sehemu moja kwenda mkoa mwingine apewe nauli ya kurudia, vinginevyo kurudi itakuwa ni majaliwa.

Mume alitakiwa ampe mkewe nauli ya kurudia kwa sababu isingewezekana kuwasiliana.

Ila sasa, inawezekana mke akakuta hali ni mbaya kijijini akazitumia pesa. Barua inabidi itumike ili kumjulisha kuwa nauli imetumika kwenye matumizi mengine.

Hata wale ambao hawakuwapa nauli za kurudia ilibidi wazitume kwa njia hiyo, au njia nnyingine iliyokuwa maarufu wakati huo, 'money telegram.'

Ukiacha yote hayo kulikuwa na njia ya mawasiliano ya kienyeji. Hii ilitumika sana kwa watu waliokuwa wakiishi mijini kutaka kuwasalimia wazazi au ndugu waliokuwa wakiishi vijijini, au kuwatumia pesa. Ilikuwa inaandikwa barua, halafu katikati yake mtu anaweza pesa, anakwenda kwenye basi lolote ambalo linapita maeneo ya kijiji chao, au tarafa, anampa dereva, kondakta, au mtu yoyote anayemfahamu na kumwelekeza kuwa akifika hapo aiangushe tu.

Kwa uaminifu mkubwa wa watu wa wakati huo, wakifika tarafa, eneo au kijiji ambacho ameelekezwa wanaiangusha bila matatizo yoyote.




Aina ya mabasi ya zamani ya abiria ambayo yalikuwa yakisafiri mikoani, tarafa na vijiji mbalimbali nchini, yaliyokuwa yakitumiwa na watu wa mijini kupeleka barua makwao na kuziangusha wanapofika maeneo hayo ili ziokotwe kwa ajili ya kupelekewa wahusika. Na kwa uaminifu mkubwa zilifika zingine zikiwa na pesa.

Wakati huo aliyeiandika, anakuwa ameandika pia jina la mzee mmoja maarufu anayejulikana na hata mtoto mdogo eneo hilo.

Yoyote anayeiokota, akisoma jina na mzee huyo atapelekewa. Mzee huyo maarufu ataichukua na kuifungua. Yeye ndiye atakayesoma na kujua ni ya nani, anatuma mtu au kuipeleka mwenyewe ikiwa na pesa kamili iliyotumwa na itafuka kama ilivyo.

Kwa kiasi kikubwa wazee hao maarufu ambao wanatumiwa kupitishia barua hizo, wanakuwa wameshazoea hali hiyo, hivyo moja kati ya kazi yake inakuwa ni kupokea barua za watu na kuzipeleka. Inawezekana baadaye walikuwa wanapata zawadi zao kama pombe, vinywaji, chakula na hata mazao kidogo, ingawa si lazima iwe mara zote.

Hayo ndiyo maisha ya zamani na mawasiliano yao ya kienyeji. Sasa unawaza kama ingekuwa sasa hivi.

Je kuna mtu kweli hivi sasa kijijini aokote barua na kuipeleka inakotakiwa? Maisha ya sasa watu wamekosa uaminifu kabisa.

Hiyo barua yoyote ambaye angeiokota angetaka kujua ndani kuna nini. Angefungua, na kukuta pesa, kitakachofuata ukakijua.

Barua inatupwa vichakani, jamaa anaondoka na pesa. Kama hina pesa atasoka kilichoandikwa, halafu ataitupa tu kwa sababu yeye siyo kazi yake kusambaza barua za watu. Ndipo tulipofikia sasa. Zamani mtu akipotea mahali au sehemu anayokwenda ni mbali, analala na kula kwa mjumbe, hadi kesho yake, au siku ambayo ataondoka bila malipo yoyote. Hiyo ilikuwa ni moja kati ya kazi za wajumbe wa zamani. Waliona fahari kufanya hivyo. Kila kitu kimebadilika hivi sasa. Teknolojia imekua kwa kasi na watu wengi sasa si waaminifu. Kwenye watu kumi, binadamu mmoja.

**Tuma meseji 0716 350534**



UCHAGUZI AFRIKA KUSINI

# ANC njiapanda, Zuma atikisa matokeo

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

CHAMA kipya cha Umkoto Wesizwe (MK) kinachoongozwa na rais wa zamani wa Afrika Kusini,Jacob Zuma, kimewashangaza wengi baada ya kufanya vizuri katika uchaguzi mkuu nchini humo.

Kulingana na matokeo yanayoendelea kutangazwa na tume ya uchaguzi, chama hicho kimepata kura kutoka kwa wafuasi wa chama kikongwe cha African National Congress (ANC), na kuwa nafasi ya tatu kwa wingi wa kura za wabunge.

Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) kinachoongozwa na Julius Malema kimeshika nafasi ya nne.

Ukuaji wa chama cha MK umekuwa mjadala ndani ya nchi hiyo kwani kilisajiliwa Septemba mwaka uliopita lakini kimepata idadi ya wabunge isiyotarajiwa.

Zuma ambaye sasa ana umri wa miaka 82, ambaye ni mwanachama wa ANC tangu akiwa na umri wa miaka 17, alitangaza Desemba mwaka jana kwamba angeweza kukipigia kura chama kingine.

Tangu wakati huo, chama cha MK kimetikisa siasa za Afrika Kusini kwa namna ambayo hakuna chama kingine kimewahi kufanikiwa kiasi hicho katika kipindi kifupi tangu kumalizika kwa mfumo wa ubaguzi wa rangi miaka 30 iliyopita.

Zuma amefanikisha hayo licha kuzuiwa kushiriki kugombea nafasi ya ubunge kutokana na kuhukumiwa kifungo huko nyuma.

Kiongozi huyo mwenye ushawishi nchini humo alihukumiwa kifungo cha miezi 15 jela kwa kosa la kudharau mahakama baada ya kukaidi agizo la kumtaka afike mahakamani hapo kukabiliana na uchunguzi wa ufisadi katika kipindi chake cha uongozi.

Kutokana na matokeo hayo, Rais Cyril Ramaphosa analazimika kujutia uamuzi huo kutokana na hasimu wake Zuma kuonyesha ana nguvu na kukitikisa chama cha ANC katika uchaguzi huo.

Chama cha ANC, kiko mbioni kupoteza wingi wa wabunge kwa mara ya kwanza tangu kilipoingia madarakani miaka 30 iliyopita, matokeo ambayo italazimika kuunda serikali muungano na vyama vingine.

Katika matokeo ya awali kutoka zaidi ya nusu ya wilaya za uchaguzi, ANC inaongoza kwa asilimia 42, ikifuatiwa na Democratic Alliance (DA) kilichopata asilimia 23.

Chama cha Umkhonto weSizwe (MK Party) kimejizolea asilimia 11 ya kura na chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) kina asilimia 10.

Matokeo ya mwisho yanatarajiwa kutangazwa mwishoni mwa wiki.

Wapiga kura wengi wameilaumu serikali ya ANC kwa kuwa na viwango vya juu vya ufisadi, uhalifu na ukosefu wa ajira nchini.

Baraza linaloheshimika la Utafiti wa Sayansi na Viwanda (CSIR) na tovuti ya News24 zimekadiria kuwa kura za mwisho za chama hicho zitakuwa karibu asilimia 42, ambazo ni chini ya 57% ilizopata katika uchaguzi wa 2019.

Kutokana na matokeo ya chama hicho, haijajulikana kama Rais Cyril Ramaphosa ataendelea kubaki madarakani kutokana na uwezekano wa kukabiliwa na shinikizo la kujiuzulu ikiwa chama kitapata chini ya 45% ya kura zote.

**BBC**



Baadhi ya wakazi wa mji wa Sake wakikimbia wakihofia mapigano baada waasi wa M23 kuuzingira mji huo juzi.
**PICHA: DW**

## Waasi M23 wauzingira mji wa Goma

**GOMA,** DRC

WAKAZI wa mji wa Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wameanza kukimbia wakati waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda wakiukaribia.

Ofisa mmoja wa serikali alinukuliwa akisema kuwa waasi wa M23 wanaukaribia mji wa Kanyabayonga uliopo kwenye njia inayoelekea Goma.

Kwa mujibu wa taarifa, mapigano makali yametokea kwenye eneo la Masisi karibu na mji wa Sake uliopo umbali wa kilometa 20 kutoka HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/hali-ya-usalama-inazidi-kuwa-mbaya-goma/a-68804485" Goma.

Majeshi la serikali ya DRC yamejaribu kuwarudisha nyuma waasi hao wa M23 wanaosemekana kuwa wameuzingira mji wa Goma ambao ni mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini.

# Trump akutwa na hatia ya uhalifu

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, amekuwa kiongozi wa kwanza wa nafasi hiyo kupatikana na hatia ya uhalifu.

Trump alipatikana na hatia ya makosa 34 ya kughushi rekodi za biashara ili kuficha malipo ya pesa kwa nyota wa filamu za ngono Stormy Daniel.

Mahakama hiyo itatoa hukumu Julai 11, siku nne kabla ya Chama cha Republican kumchagua mtu ambaye atagombea nafasi ya urais katika mkutano mkuu wa chama.

Hata hivyo, Trump amepinga uamuzi huo na kutangaza kuwa angefanya mkutano na waandishi wa habari kuelezea masikitiko yake.

Athari ya uamuzi huo wa kihistoria bado haijukuwa wazi, kuhusu athari zinatakazojitokeza nafasi yake ya kuwania urais.

Kambi ya Rais Joe Biden ilitoa taarifa, na kuwakumbusha wapiga kura kwamba njia pekee ya kumshinda Trump ni kwenye sanduku la kura na sio chumba cha mahakama.

Mmoja wa mawakili wakuu wa Trump, aliambia Fox News kwamba timu ya wanasheria wanatarajia kukutana ili kukata rufaa.

"Kila kipengele cha kesi hii kiko tayari kwa rufaa.Tutakata rufaa haraka tuwezavyo." alisema wakili huyo Will Scharf.

Wakili mwingine katika timu ya wanasheria wa Trump, Todd Blanche, pia alijitokeza na kueleza kuwa hakutendewa haki.

"Tumekuwa tukisema kwa zaidi ya mwaka mmoja kwamba hatukutendewa haki huko Manhattan," alisema.

Baada ya siku mbili za mashauriano katika mahakama hiyo, Donald Trump alikutwa na hatia ya mashtaka yote katika kesi yake ya uhujumu uchumi.

Wabunge wa chama cha Democratic na baadhi ya wakosoaji wakubwa wa Donald Trump walituma ujumbe kupitia mtandao wa X, ambayo zamani ilikuwa Twitter, kwa kusema kuwa haki imeshinda.

"Leo, majaji kumi wa Marekani walimpata na hatia rais wa zamani makosa kadhaa. Licha ya jitihada zake za kuvuruga, kuchelewesha, na kukanusha, haki imetendeka dhidi ya Donald Trump vivyo hivyo. Na utawala wa sheria ulitawala," Mwakilishi wa California Adam Schiff aliandika. Schiff.

"Majaji wamezungumza. Haki imeshinda," Mwakilishi mwingine Jim Clyburn, mwanademokrasia kutoka Carolina Kusini, aliandika kwenye mtandao wa X.

Mwakilishi wa Washington Pramila Jayapal, mwenyekiti wa Baraza la Maendeleo la Congress, aliuita uamuzi huo kuwa ni wakati muhimu kwa uwajibikaji nchini Marekani.

**BBC**




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (wa tatu kushoto), akizindua kifaa kitakachotumia teknolojia ya akili bandia kufuatilia hali za wagonjwa wa moyo wakiwa nyumbani, baada ya kufanyiwa upasuaji katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), katika hafla iliyofanyika katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi usiku. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania yakwaa ugavana Benki ya Maendeleo Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kushika nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji mbadala (Alternative Executive Director) katika Kundi la Magavana wa Afrika Mashariki katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kuanzia Agosti, 2024.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-Maamry Mwamba, aliyasema hayo kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa mkutano wa kawaida wa magavana wa Kundi la Nchi za Afrika Mashariki ambao ni wanachama wa AfDB.

Mkutano huo ni maandalizi ya mikutano ya mwaka 2024 ya Bodi ya Magavana (Mawaziri wa Fedha kutoka nchi wanachama) wa benki hiyo inayofanyika Nairobi, Kenya.

Dk. Mwamba alisema AfDB imeweka utaratibu wa mzunguko wa uongozi katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki ambao ni Mkurugenzi Mtendaji na Mshauri na kwa upande wa Tanzania, kunakuwa na Mkurugenzi Mtendaji mbadala.

"Katika mkutano huu tumezungumzia pia mzunguko wa viongozi ambao ni Mkurugenzi Mtendaji na Mshauri na sisi Tanzania kuanzia mwezi Agosti, 2024 tutashika nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji mbadala katika Benki hiyo ambaye atakuwa anachukua nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji anapokuwa anapata udhuru,"alisema Dk. Mwamba.

Aidha, Dk. Mwamba alisema kuwa mkutano huo ulijadili kuhusu mabadiliko ya tabia nchi ambayo hivi karibuni yamekuwa yakisababisha maafa mbalimbali na kukubaliana kuanzishwa kwa mfuko wa maafa ambao utakuwa unasaidia nchi zitakazo athirika na mabadiliko hayo ikiwemo mvua zisizotarajiwa za El-nino.

"Tumejadili pia kuhusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kuongeza mtaji. Lakini pia nchi zilizopata majanga ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua nyingi zilizojitokeza mwaka huu pia itakuwa ajenda itakayojadiliwa katika mkutano mkuu," aliongeza Dk. Mwamba.

Mkutano wa kundi la nchi za Afrika Mashariki ambao umeshirikisha wajumbe kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Ethiopia, Somalia, Afrika Kusini, Sudan, Eritrea na Shelisheli ni utangulizi wa Mkutano wa 59 wa mwaka wa AfDB.

# Waaswa kuchunguza kabla ya kukopa

**Na Josephine Majula,** KAGERA

DIWANI wa Mutukula, Haji Chakula, amewataka wananchi kufanya uchunguzi na kujiridhisha na taasisi ya fedha anayotaka kuchuchukua mikopo kama imesajiliwa kisheria ili kuepuka kuingia kwenye matatizo.

Pia amewataka wananchi kusoma kwa kina masharti na kuelewa, ikiwamo kujua kiwango cha riba kwa mkopo husika kabla ya kufanya uamuzi wa kuchukua fedha.

Alisema hayo baada ya kupata elimu ya masuala ya fedha inayotolewa na Timu ya Wataalamu ya Wizara ya Fedha iliyoko mkoani Kagera kuelimisha wananchi masuala ya fedha na namna ya kuepuka mikopo umiza.

"Nawasihi sana wananchi wangu msiwe wepesi kukimbilia kuchukua fedha kabla ya kusoma mkataba na kuelewa masharti ya mkopo hata kama una uhitaji wa fedha hii itasaidia kupunguza kesi zinazoendelea katika kata yetu,"alisema Chakula.

Mjasiriamali mkazi wa Kata ya Mutukula wilayani Missenyi, Anna Domisian, alisema kabla ya kupata elimu ya fedha, alikuwa akichukua mikopo kwa mazoea bila kusoma mkataba ambayo ilikuwa ikimsababishia matatizo wakati wa kurejesha.

"Elimu niliyoipata leo itanikomboa kiuchumi lakini itanisaidia kuepukana na migogoro na watoa huduma. Elimu hii nitaitumia kuwaelimisha wanakikundi wenzangu umuhimu wa kusoma mkataba kila karatasi na kuhakikisha wanaelewa ndipo wasaini," alisema Domisian.

Ofisa Mwandamizi Uchambuzi wa Masuala ya Fedha Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Gladness Mollel, alitoa elimu kwa wananchi kuhakikisha wanatia saini kila karatasi ya mkataba wanapochukua mkopo ili kuepusha kuongezwa kwa karatasi nyingine yenye masharti magumu ambayo hayatekelezeki.

Mkurugenzi wa taasisi ya mikopo mkazi wa Kata ya Mutukula, Dunstan Sebastian, aliwashauri watoa huduma za fedha kuwaelimisha wakopaji kabla ya kuwapa mikopo ili waelewe masharti ikiwamo kiwango cha riba wanachopaswa kurejesha kwa mujibu wa sheria.

Pia aliwatata kuhakikisha kabla mteja hajasaini mkataba wa mkopo wawe wamesoma na kuelewa wajibu wake, jambo litakalopunguza migogoro baina ya taasisi ya fedha na mkopaji.

"Tunaishukuru serikali kupitia wizara ya fedha kuona umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi, elimu hii ikiwafikia wananchi wote itasaidia kupunguza kama sio kumaliza migogoro inayoendelea nchini," alisema Sebastian.

Timu ya wataalamu hao ni kutoka Wizara ya Fedha ambao wameambatana na taasisi zingine za serikali zikiwamo Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

# Kampuni yazuiwa kununua mazao kudaiwa madeni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zaynab Telack, ameipiga marufuku kampuni ya Listram kununua mazao kutokana na kutolipa fedha za wakulima wa kata ya Mikoma, wilayani Kilwa msimu uliopita.

Kampuni hiyo inadaiwa kutokuwalipa wakulima hao Sh. 44,067,579 baada ya kuiuzia korosho kupitia soko la awali.

Zuio hilo alilitoa juzi wakati wa kikao cha wadau wa kilimo na ushirika kutathmini msimu wa korosho 2023/24, kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Shule ya Sekondari Nyangao, Halmashauri ya Mtama.

Telack aliweka zuio hilo baada ya mdau wa kilimo, Juma Kapera, kutaka kufahamu hatima ya malipo ya wakulima wa Kata ya Mikoma, kwa kuchukuliwa korosho zao na Kampuni ya Latram msimu uliopita bila kulipwa fedha zao.

Katika uamuzi huo, Telack alisema kutokana na kampuni hiyo kutolipa wakulima fedha zao zilizotokana korosho alizochukuwa msimu uliopita bila kuwalipa, hana sababu za kuendelea kununua mazao ndani ya mkoa wa Lindi.

"Kitendo cha kutowalipa wakulima fedha zao ni ukatili uliopitiliza dhidi ya wavuja jasho wasio na hatia yoyote," alisema Telack.

Mkuu huyo wa mkoa alimwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kumfuatilia mmiliki wa kampuni na kumchukulia hatua za kisheria.

Kutokana na malalamiko yaliyotolewa na mdau huyo, uongozi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) Kanda ya Mtwara kupitia Mkurugenzi Mkuu, Francis Alfred, umebeba mzigo wa kuwalipa wakulima wa kata ya Mikoma.

**"Kitendo cha kutowalipa wakulima fedha zao ni ukatili uliopitiliza dhidi ya wavuja jasho wasio na hatia yoyote," alisema Telack.**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-15

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Alichukua simu ya marehemu mchumba wake ambayo aliikuta siku ile alipokwenda nyumbani kwake na kutomkuta, kabla ya kupata taarifa ya kifo chake kesho yake, ikidaiwa amenguka akiwa anafanya mazoezi huko Tabata, lakini baadaye ndiyo ikasemana yeye ndiyo amemuua.

Akaanza kukagua meseji mbalimbali zilizokuwa zikitumwa. Alifanya hivyo ili kung'amua ambazo zingempa mwanga kuwa ni nani wanaweza kuwa nyuma ya tukio hilo.

Kati ya zote, akapata meseji tano ambazo zilionyesha za wanaume waliokuwa wanamtaka na kumfuatilia kwa muda mrefu.

Ndipo alipogundua kuwa Mariamu alikuwa mwanifu mno kwake, lakini meseji zote zilikuwa zinamtuhumu kwa kumpenda mtu kapuku, asiye na kitu ambaye ni yeye.

Ikaenda mbali sana, meseji zile zitaonyesha kuwa watu hao watamuua yeye, na baadaye kupata urahisi wa kubaki naye.

Lakini ipo meseji ambayo Mariamu aliwajibu kuwa kama wakimuua Kamal, wakitengemea ndiyo atawakubali basi wamenoa.

"Mtoto wa watu hana kosa, unataka kumuua kwa sababu gani, kwa sababu ya pesa zako, utajiri wako, kumbuka ukifanya hivyo tu, nakwenda kukuripoti polisi, halafu na mimi najiua. Siwezi kuona mtoto wa watu ameuawa kwa sababu yangu, halafu mimi nikaendelea kula raha duniani. Kama huko kuna kuoana, basi tukakwenda kuoana paradiso." Ilikuwa ni meseji ambayo aliituma kwa mtu mmoja ambayo yeye mwenyewe Kamal hakumfahamu.

Ni kweli Kamal alijua marehemu, Mariamu anampenda, lakini hakutegemea kwa kiwango kile kiasi cha hata kukubali kutoa uhai wake.

Pamoja na hayo hakushangaa sana kuhusu meseji zile za wanaume, kwani alijua mchumba wake alifuatiliwa na kutomgozwa na wanaume wengi ambao ni wazito, wafanyabiashara wakubwa, matajiri, wenye vyeo kama vile maneneja na wakurugenzi kutokana na urembo wake.

Alijua kabisa kama marehemu Mariamu angekuwa mtu wa tamaa, angekuwa na pesa nyingi sana, asingekuwa vile hata kama angekuwa anachepuka.

Asingekosa gari kali la kutembelea na vitu vingine kwa thamani ambavyo warembo wengi wanavyo.

Pamoja na kwanza bado kila mtu alikuwa anaishi kwake, lakini alikuwa




**Mariamu akaangua kicheko ambacho hakikuwa halisi. "Yaani unaupenda uhai wako kuliko mimi ninavyoupenda wangu?" "Kwa nini unaongea hivyo halafu unacheka?" Kamal naye akauliza.**

sehemu ya maisha yake, hivyo alifahamu kipato chake, na hata alivyokuwa wakati mwingine akihangaika kupata mkopo, na mahitaji mengine kwa ajili ya maisha ya biashara zake.

Anakumbuka hata yeye mwenyewe tu ameshawahi kuandikiwa meseji kibao za vitisho na watu hao ili aamuache kwa sababu waliona ndiye kikwazo.

Vitisho vilikuwa vikubwa, wengine wakisema watamuwekea sumu kwenye chakula, vinywaji, kumkodishia majambazi, kumgonga na gari, baadhi walitishia hata kumuendea kwa waganga wa kienyeji.

"Haiwezekani wewe kapuku tu ukawa na mtoto mzuri kama yule, tunamuomba jiondoe kabisa, muache ili wakubwa tule raha. Ukibisha tutajua la kukufanya, maiti yako haitapelekwa kwa ndugu zako, tutawapeleka samaki baharini, au ndege au wanyama porini." Ni moja kati ya meseji anazozikumbuka ambazo zilimyong'onyesha sana. Akaogopa, akavunjika nguvu na akaazimia kumuacha.

Siku moja akamwita nyumbani kwake na kumweleza maneno ya kukatisha tamaa, kwani alijua siku yoyote anaweza kuuawa.

Alipoingia ndani alimkuta Kamal akiwa myonge. Hakuwa na furaha kama siku zote. Hiyo ilimtisha Mariamu. Alikuwa amekaa kwenye kochi amejikunyata. Kila mtu anamjua mtu wake. Kwa hali ile alikuwa kuna namna. "Hivi mwenyetu una nini leo, unaumwa?" Akauliza, kwani hata uitaji ule ulikuwa wa ghafla sana.

Hakujibu mapema, kitu ambacho kilimthibitishia Mariamu kuwa kuna jambo. Akaonyesha ishara kuwa akae kwenye kocha pembeni yake. Akamtazama usoni na kumuuliza tena."Mpenzi, kwani kumetokea nini?"

"Mariamu mchumba wangu, nyota nadhifu wa moyo wangu, naomba unikubalie hili nitakalokuomba, kama ulivyonikubalia tukawa sote." Akaanza Kamal kwa maneno tata.

"Nikukubalie? Nikukubalie nini tena?" Akauliza Mariamu. "Wewe sema tu kama utanikubalia." Mariamu alianza kuhisi kuwa kuna jambo lisilo la kawaida.

"Kwa sasa najijutia mpenzi, nimejitosa ndani ya moto na matatizo, kuwa na wewe umekuwa nongwa, kwao ni kero kwa wasiopenda niwe na wewe."

Kwa mbali ni kama alianza kumuelewa. Kwa sababu ni kweli kuna wasiopenda wao kuwa pamoja. Halini ni hilo tu au kuna lingine? Kabla hajasema lolote, Kamal aliendelea.

"Mariamu, wewe ni mrembo, Mungu hakukubakisha kitu, ni mzuri, mrembo una umbile zuri, lakini uzuri wako na ufukara kwao ni vibaya, roho zinawauma."

"Najua hilo mpenzi wangu, na hata wewe unalijua muda mrefu, lakini hili ndiyo limekufanya uniite huku ghafla hivi Kamal?" Akauliza. "Hapana Mariamu, nilichokuitia ndiyo naanza kukisema."

Mariamu alibaki mdomo wazi, alishindwa kuongea chochote, akimuacha mpenzi wake aendelee anachotaka kuongea.

"Ninachokuomba sasa Mariamu, imenibidi, ni bora nilivue mimi hili penzi, niwape nafasi waoamini umeshushwa kwa ajili yao si vyema uwe na mimi." "Unasemaje wewe?" Akauliza Mariamu kwa sauti ya ukali kidogo kama vile hakubaliani na anachokiongea Kamal.

Haikumfanya Kamal kuendelea kile alichokuwa anakifikirika moyoni mwake. Hakushtuka, wala na wewe kuonyesha hasira

"Ingawa tumeaopa tusingetengena nawe mpaka kifo kabla hata hatujafunga ndoa, lakini inatubidi tutengane, niwaridhishe wale wabaya kwenye pendo letu." Kamal alimaliza na kushusha pumzi nzito akionekana alichokuwa akitaka kukitapika ameshakitoa na sasa imebaki uamuzi wa Mariamu.

Mariamu alimtazama Kamal kwa dakika moja nzima bila kuongea kitu chochote, halafu akamuuliza.

"Hivi wewe mzima kweli?" "Mzima kama chuma cha pua." "Sasa haya maneno unayoongea yanatoka moyoni mwako, au umeambiwa uyaseme?" "Yanatoka moyoni mwangu kwa sababu hata nami naupenda uhai wangu." "Wamekufuata na kukutishia?"

"Mariamu, nimepokea meseji za vitisho kutoka kwa watu tofauti tofauti ambao siwajui na kila mara wanafanya hivyo. Na ukienda kuangalia zile namba kwenye simu hazionyeshi jina la mtu yoyote, na hata ukipiga hazipatikani. Kwa hiyo hapa unaponiona maisha yangu yapo hatarini. Siku yoyote na muda wowote naweza kuuawa."

Mariamu akaangua kicheko ambacho hakikuwa halisi. "Yaani unaupenda uhai wako kuliko mimi ninavyoupenda wangu?" "Kwa nini unaongea hivyo halafu unacheka?" Kamal naye akauliza.

"Kama kuogopa kifo basi mimi ningekuwa namba moja. Mimi nina meseji nyingi za vitisho zaidi yako. Nimetishiwa mimi kuuawa ili nikuache, nimewaambia nyie niueni tu, lakini hilo haliwezekani. Wamesema watakuua ili wanichukue kama hizo ulizonazo, nimewaambia hata mkimuua, mtakayempata ni marehemu Mariamu, siyo aliye hai, kwa sababu kama akifa Kamal na mimi najiua."

**Itaendelea Jumamosi**

# YANGA VINARA MASHUTI KULENGA LANGO 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga na Azam zikiwa Zanzibar kwa ajili ya mechi ya fainali ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, timu hizo zimeweka rekodi tofauti katika Ligi Kuu mapema wiki hii.

Yanga imeweka rekodi ya kuwa kinara wa kupiga mashuti mengi yaliyolenga lango, huku Azam FC waking'ara kwa kupiga mashuti yaliyotoka nje.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu za michezo, na chanzo kingine ndani ya Bodi ya Ligi, Yanga imepiga mashuti 205 ambayo yamelenga lango, ikiwa ndiyo timu iliyoongoza kufanya hivyo, ikifuatiwa na Azam FC, ambayo mashuti yake 196 yalilenga, huku Simba ikishika nafasi ya tatu, yenyewe ikitandika mashuti 177 yaliyoenda kwenye usawa na lango.

Tabora United, ndiyo iliyopiga mashuti machache yaliyolenga, ikifanya hivyo mara 93 tu, ikifuatiwa na Coastal Union mara 96, na Geita Gold ikipiga mara 99.

Kwa mashuti ambayo yalikwenda nje, Azam FC ndiyo kinara wao, ikifanya hivyo mara 220, ikifuatiwa na Mtibwa Sugar iliyopiga mashuti fyongo mara 209, Yanga ya tatu ilipiga makombora 192, huku Mashujaa FC ikipiga mashuti machache zaidi yaliyotoka nje, ikifanya hivyo mara 125.

Takwimu zinaendelea kuonyesha mabeki wa Coastal Union ndiyo waliookoa hatari nyingi zaidi langoni mwao msimu huu, ikifanya hivyo mara 334, Mashujaa FC na Prisons zikiondoa hatari langoni mwao mara 321.

Mabeki wa Yanga wameokoa hatari machache zaidi katika ligi hiyo iliyomalizika, wakifanya hivyo mara 157, wakifuatiwa na wa Simba wakiokoa mara 177.

Ihefu FC, kwa mujibu wa takwimu zetu na vyanzo kutoka Bodi ya Ligi, ndiyo timu ambayo viungo wao wa kati walizuia hatari nyingi kuelekea langoni mwao.

Waliharibu mpango ya wapinzani na kunasa mipira mara 491, wakifuatiwa na Prisons mara 445, KMC mara 441, huku viungo wa JKT Tanzania wakishika nafasi ya mwisho kwa kunasa mipira ya wapinzani, wakifanya hivyo mara 331, wakifuatiwa na Tabora United, mara 333.

Hata hivyo Mtibwa Sugar na Geita Gold zimeshuka daraja moja kwa moja wakati Tabora United na JKT Tanzania zitatakiwa kupambana kujinusuru kwa kujaribu tena bahati kwa kucheza michezo ya mtoano.




Nahodha wa TSC Queens, Nasra Rajabu (kushoto), akipokea Kombe baada ya timu yao kutwaa ubingwa wa Ligi ya Soka ya Wanawake Mkoa wa Mwanza baada ya kuichapa Talented Girls mabao 5-2 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHANEZA kuchaguana Juni 9

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

UCHAGUZI Mkuu wa Chama Cha Netiboli Zanzibar (CHANEZA) umepangwa kufanyika Juni 9, mwaka huu, imefahamika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ), Muhidini Masunzu Yasin, alisema tayari zoezi la uchukuaji fomu limeanza na litamalizika leo katika ofisi za kiongozi huyo wa kamati zilizoko katika Hospitali ya Polisi Ziwani.

Yasin alitaja nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo ni ya Rais, Makamu wa Rais wawili (Pemba na Unguja), Katibu Mkuu, Makatibu Wasaidizi (mmoja kutoka kila upande), Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

"Kutakuwa na ada kwa ajili ya uchukuaji fomu hizo, kwa watakaogombea nafasi ya Urais, Makamu wa Rais, Katibu, Katibu Msaidizi na Mweka Hazina ni Sh. 100,000 huku nafasi zilizobakia ni Sh. 75,000," alisema Yasin. Aliongeza kamati itapitia fomu zote zilizorejeshwa na keshokutwa kutakuwa na usaili wa wagombea.

Alisema muda wa kuweka pingamizi wa wagombea ni Juni 4, siku inayofuata majina ya wagombea waliopitishwa wataanza kampeni ambazo zitamalizika ifikapo Juni 8, mwaka huu.

## Wadau Dodoma Jiji kicheko, watoa neno

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yao kufanikiwa kubaki katika Ligi Kuu, mashabiki wa Dodoma Jiji FC wamewakumbusha viongozi wao kufanya usajili mzuri kuelekea msimu mpya ili kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

Meneja wa Uwanja wa Jamhuri, Anthony Nyembela, ambao hutumiwa na Dodoma Jiji kama uwanja wa nyumbani, ameonyesha furaha yake kama mkazi wa jiji hilo, akisema hiyo itawapa fursa kuzitazama mechi nyingine 15 za msimu ujao wa ligi.

"Kubakia Ligi Kuu timu yetu ya Dodoma Jiji imetupa furaha sana watu wa Dodoma, tuna uhakika wa kuziona tena mechi 15 za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Tena tunashukuru msimu huu haujawahi kufungiwa hata mara moja msimu huu, mechi zote walichezea hapa, tunaahidi kufanya maboresho ili msimu ujao mechi zote zipigwe hapa," meneja huyo alisema.

Simon Simon, mmoja wa mashabiki wa timu hiyo, aliwataka viongozi wa Dodoma Jiji na Halmashauri ya Jiji hilo kufanya usajili wa nguvu kuelekea msimu ujao ili angalau kuona wanapata nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tunataka angalau sasa msimu ujao tumalize nafasi ya tatu au nne ili tucheze sasa mechi za kimataifa, Halmashauri ya Jiji la Dodoma sasa ielekeze nguvu kwa ajili ya kusajili wachezaji wazuri, iendelee kushirikiana na wamiliki wa uwanja ili kiwe kwenye hali nzuri, ili hata hizo mechi za kimataifa zipigwe kwenye uwanja huu," alisema Simon.

Aliongeza anaamini uwanja huo ukiboreshwa zaidi, hata timu nyingine zinaweza kuhamia Dodoma na kuwapa fursa zaidi mashabiki wa soka wa jiji hilo kufurahia mchezo huo.

Dodoma Jiji ilimaliza mechi yake ya mwisho kwa kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Mashujaa FC, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma lakini kichapo cha mabao 2-0 ilichokipata JKT Tanzania kutoka kwa Simba kiliwaokoa na kumaliza ikiwa katika nafasi ya 12, baada ya kuvuna na pointi 33.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Francis Baraza, alisema ligi ilikuwa ngumu na hii imetokana na kila timu kuwekeza katika vikosi vyao.

"Uwekezaji mzuri ndio husaidia timu kupata matokeo mazuri, hakuna mechi ambayo ilikuwa rahisi kwa timu yoyote msimu huu, tumemaliza msimu salama, tunaenda kujipanga kwa ajili ya msimu mpya, tutajiimarisha katika kila idara," Baraza aliongeza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHALOBAH ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua beki wa Chelsea, raia wa England, Trevoh Chalobah, mwenye umri wa miaka 24. (***Independent***)

### DIAZ, GOMEZ WATAJWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27 na mlinzi wa England, Joe Gomez (27), wanawaniwa na klabu za Ligi ya Saudia huku zinatazamia kuwapata wachezaji wachanga msimu huu. (***Mail***)

### RICHARLISON, EMERSON KUUZWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inapokea ofa ya kuwauza wachezaji wa kimataifa wa Brazil. Wazezaji hao ni mshambuliaji Richarlison mwenye miaka 27 na beki Emerson Royal (25). (***Standard***)

### SESKO KUTUA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 20 anapendelea kuhamia Arsenal msimu huu wa joto. (***Mirror***)

### EVERTON KUIKAMUA UNITED

EVERTON imeiambia Manchester United kusahau mpango wa kumsajili beki wa England wa chini ya umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite, kwa bei nafuu. The Toffees wanataka pauni milioni 40 ili kumwachia nyota huyo. (***Mirror***)

### UNITED KUMBANA MASON

MANCHESTER United inafikiria kuongeza mkataba wa mshambuliaji, Mason Greenwood, zaidi ya mwaka mmoja ili kuhakikisha mauzo ya kudumu yanakamilika. Juventus, Napoli, Atletico Madrid na Borussia Dortmund zinamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. (***i Sport***)

### WEST HAM, PALMEIRAS KUTETA

KLABU ya West Ham ipo katika mazungumzo na Palmeiras kuhusu kumnunua kiungo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, Luis Guilherme. (***Fabrizio Romano***)

### HARTMAN ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Quilindschy Hartman, mwenye umri wa miaka 22, kutoka Feyenoord. (***Telegraph***)

### BROJA AKARIBIA MONACO

MONACO iko mbele zaidi kuliko Watford au AC Milan katika mbio za kuwania huduma ya mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja. (***L'Equipe***)

### BELLINGHAM KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inajadiliana na Sunderland kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji, Jobe Bellingham, mwenye umri wa miaka 18, ambaye pia anaweza kucheza katika safu ya kiungo. (***Standard***)

### EVERTON YAMFUATA BARKLEY

EVERTON imeonyesha nia ya kutaka kumsajili tena kiungo wa kati, Ross Barkley, mwenye umri wa miaka 30 kutoka Luton Town.(***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LUNIN NJE MADRID IKIIVAA DORTMUND

**Ni katika fainali ya UEFA itakayochezwa leo kutokana na...**

**LONDON,** England

GOLIKIPA chaguo la kwanza kwa sasa wa Real Madrid, Andriy Lunin, amejiondoa katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund itakayochezwa leo baada ya kutosafiri kwenda London pamoja na wachezaji wengine.

Lunin amekuwa kipa bora msimu huu tangu apate nafasi ambayo haikutarajiwa wakati Thibaut Courtois alipopata jeraha la muda mrefu hapo Agosti, lakini alikuwa na shaka kwa fainali wiki nzima.

Mchezaji huyo wa Ukraine, ambaye hivi karibuni ameachia nafasi yake ya LaLiga kwa Courtois aliye fiti tena lakini alidaka mwenye mechi zote mbili za nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Bayern Munich, alikosa mazoezi ya Jumatatu, Jumanne na Jumatano kutokana na kuumwa mafua.

**Kikosi cha Madrid kilipanda ndege kuelekea England juzi bila Lunin.**

Gazeti la Marca liliripoti kipa huyo, anayeonekana ni mwenye hatari ya kuwaambukiza wenzake alitarajiwa kusafiri peke yake jana au leo.

Lakini uwezekano wa kucheza katika hali kama ni mdogo na alionekana kuthibitisha katika chapisho la Instagram juzi jioni amepoteza pambano hilo.

"Samahani siwezi kujiandaa kwa mchezo muhimu zaidi wa timu kwa msimu na muhimu zaidi maishani mwangu," aliandika Lunin akiwaambia wafuasi wake wa milioni 3.3.

Courtois kucheza katika fainali hii katika msimu huu kunaweza kumpa taji lake la pili la Ulaya.



# GREALISH 'ALIAMSHA' MAN CITY

**MANCHESTER,** England

KIUNGO mshambuliaji wa England, Jack Grealish, huenda akachana na mabingwa Ligi Kuu England, Manchester City, kufuatia madai ya kukiukwa kwa mkataba wake.

Grealish amekuwa hapati nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza cha City, kama ilivyotarajiwa wakati akisajiliwa huko Etihad akitokea Aston Villa.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 28, anatarajia kufanya mazungumzo na Kocha Pep Guardiola, kuhusu mustakabali wake klabuni hapo ili kufahamu kama atarejea kwenye kikosi cha kwanza msimu ujao.

Gazeti la The Sun limeripoti Grealish amejipanga kuhoji muda wa kucheza ambao unaendelea kupungua kila kukicha, huku asilimia kubwa akitumika kama mchezaji wa akiba.

Hata hivyo, Tovuti ya SunSport imeripoti miamba ya Ujerumani, FC Bayern Munich inafikiria kumsajili winga huyo endapo mazungumzo yake na Guardiola yatashindwa kuzaa matunda.

Ingawa inaelezwa kocha huyo kutoka nchini Hispania bado ana nia ya kufanya kazi ya Grealish.

## Arteta kupewa mkataba mpya



**LONDON,** England

UONGOZI wa Arsenal una mpango wa kumpa mkataba mpya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mikel Arteta na kumsajili mshambuliaji kutoka Slovenia na RB Leipzig ya Ujerumani, Benjamin Sesko.

Gazeti la The Mirror limeripoti hatua ya Arteta kutarajiwa kusaini mkataba mpya, itatumika kama silaha ya kumvuta mshambuliaji huyo mwenye umri wa 20, ambaye kwa sasa anaongoza katika orodha ya wanaopigiwa upatu wa kusajiliwa hapo Uwanja wa Emirates.

Gazeti hilo limeandika: „Mikel Arteta yuko katika hatua nzuri kukamilisha mpango wa kusaini mkataba mpya, kufuatia mazungumzo kati yake na uongozi wa Arsenal kwenda vizuri.

Mkataba wa sasa wa kocha huyo kutoka nchini Hispania umebakisha mwaka mmoja, huku akijidhihirisha kuwa mmoja wa makocha wanaochipukia barani Ulaya.

Kwa sasa Arsenal ipo sokoni kutafuta mshambuliaji mpya huku Sesko akiongoza kwenye orodha iliyowasilishwa mezani kwa viongozi klabuni hapo.

## Son, Spurs mambo mazuri

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur inajipanga kumfunga, Son Heung-min, kwa kumpa mkataba wa mwaka mmoja zaidi, na hivyo kufuta kabisa uwezekano wa nahodha wa timu hiyo kuelekea kwenye mlango wa kutokea msimu huu wa joto.

Son alichukua kiwango kipya cha uwajibikaji 2023/24 kufuatia kuondoka kwa Harry Kane na akafunga mabao 17 ya Ligi Kuu England, kufikia idadi yake ya pili bora ya msimu mmoja kwenye kinyang'anyiro hicho.

Lakini nyota huyo wa Korea Kusini atafikisha miaka 32 kabla ya msimu ujao kuanza, na umri wake unatosha kuweka uvumi juu ya uwezekano wa kuhamia Saudia.


Son ambaye hivi karibuni ataingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wa muda mrefu ambao alisaini mnamo 2021, lakini The Athletic limeandika chaguo la mwaka mmoja la kurefusha hadi 2026 litatazamwa.

Inamaanisha tarehe mpya ya kumalizika kwa mkataba wake itasogezwa hadi wiki moja kabla ya siku yake ya kuzaliwa.

Msimu uliopita wa kiangazi, Son alifichua kwa msisitizo hakuwa na nia ya kuhamia Saudi Arabia.

„Kama nilitaka kwenda huko, nisingekuwa hapa!" alisema mchezaji huyo katika mkutano na waandishi wa habari wakati wa ziara ya Tottenham ya maandalizi ya msimu mpya nchini Australia.

„Ninapenda kucheza soka. Ni wazi fedha pia ni muhimu lakini nina ndoto ya kumalizia soka katika Ligi Kuu England."



# SIMBA SC, YANGA, AZAM FC ZAKUMBUSHWA USAJILI CAF

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limezitaka timu zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao kufanya usajili mzuri kwa ajili ya kufanya vyema katika michuano hiyo na kuipa heshima nchi, imeelezwa.

Mabingwa wa Ligi Kuu, Yanga, Azam FC, Simba zote za Dar es Salaam na Coastal Union ya jijini, Tanga zinatarajiwa kupeperusha bendera ya Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la S oka Afrika (CAF).

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi, alisema endapo timu hizo hazitafanya usajili bora, zitashindwa kuonyesha ushindani na kufanya vyema katika mashindano hayo.

Madadi alisema anaamini usajili bora utasaidia kuzipa matokeo mazuri na hatimaye kila timu kufikia malengo yake.

„TFF tunazishauri timu zote zinazokwenda kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao kuhakikisha zinasajili wachezaji ambao watawapa mafanikio kwa kufanya vizuri katika michezo ya kimataifa," alisema Madadi.

Alizipongeza timu zote ambazo zimepata nafasi ya kushiriki mashindano hayo na kusema wamepata tiketi hiyo kutokana na juhudi walizozionyesha katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika mapema wiki hii.

Kiongozi huyo pia amewataka wachezaji wote walioshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Ligi ya Championship kutuma vizuri muda huu wa mapumziko kwa kufanya mazoezi ya ziada.

Alisema msimu uliopita ulikuwa na msisimko mkubwa kutokana na ushindani ulionyeshwa na timu zote.

„Msimu uliopita ulikuwa na ushindani na hali hiyo imefanya ligi yetu kuonekana yenye ubora, vilevile tunawashukuru wadhamini wote kwa kazi nzuri waliyoifanya, „ Madai aliongeza.

Mtibwa Sugar na Geita Gold zimeshuka daraja moja kwa moja wakati Tabora United na JKT Tanzania zinasubiri kucheza michezo ya mtoano kwa kupambana na timu kutoka Ligi ya Championship.

## Yanga SC, Azam FC tambo zatawala

INATOKA UK. 24

na hii ni kwa ajili ya kuanza ‚kusuka' upya kikosi cha msimu mpya.

„Tukishamaliza mechi yetu ya fainali tunatarajia kuanza kutangaza wachezaji ambao hatuwahitaji kueleke msimu mpya, na wale tutakaowaongeza tutawaweka hadharani kwa lengo la kuwapa burudani mashabiki wetu.

Kwa kifupi wachezaji wako tayari, wana morali ya hali ya juu, tunajua mchezo utakuwa mgumu, lakini kwa sasa wachezaji wetu wamejenga mazingira ya kujiamini zaidi," alisema Hasheem Ibwe, Ofisa Habari Msaidizi wa Azam FC.






Mshindi wa Jackpot bonus kutoka SportPesa, Alphonce Fungo, akiwa amekabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 5.3 baada ya kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Fungo ashinda Bonus ya Jackport SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Ilala jijini, Dar es Salaam, Alphonce Fungo amejishindia Sh, milioni 5.3 kama bonus ya Jackpot ya SportPesa baada ya kupatia kwa usahihi mechi 10 kati ya mechi 13 alizobashiri.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za SportPesa, Alphonce alisema alianza kucheza na SportPesa mwaka 2023.

„"Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2023 mwezi kama huu wa tano, na katika kipindi chote hiko nimefanikiwa kushinda kiasi tofauti kama Sh. 800,000 au 700,000 au Sh. 300,000 na kiasi cha mwisho ni hiki ambacho nimebahatika wiki iliyopita ni zaidi ya Sh. milioni tano ambazo zote nimeshinda kwenye Jackpot ya mechi 13.

SportPesa nimeifahamu muda mrefu, kwa mara ya kwanza niliona nikiwa Mbeya, mara nyingi nikiwa na rafiki yangu sehemu ya kazi alikuwa akitumia muda mwingi kwenye simu yake, siku moja nilimuuliza huwa nakuona uko busy sana na simu yako, ndipo aliponiambia huwa natumia muda mwingi kupanga mikeka, ndipo nilipoanza kujifunza kucheza Jackpot, pia SportPesa ni kampuni ambayo haina longo longo kwenye ulipaji pale ambapo unakuwa umeshinda.

Kuhusu mkeka alioshinda, Alphonce alisema huwa anachukua masaa mawili hadi matatu kuzikagua timu na kujua timu ipi ataipa ushindi.

„Mimi napenda kutumia muda mrefu wa kuangalia kwanza timu na kuzichambua kabla sijaweka mkeka wangu, na huwa natumia masaa mawili hadi matatu kupangilia mkeka wangu mara nyingi huwa naweka mikeka 20 hadi 30.

Anaendelea kusema wakati anasubiri matokeo alikuwa na shauku kubwa sana baada ya kuona mkeka mmoja ameshinda mechi tisa, hapo ndio alianza kuamini anaweza kuwa mshindi wa jackpot au ataweza kupata bonus.

Nakumbuka mechi ya mwisho inachezwa nilikuwa maeneo ya nyumbani kwenye mida ya saa sita usiku, nilikuwa nimekaa nasubiria matokeo ya ushindi, na hapo hapo meseji iliingia, kwakweli nilifurahi sana, alisema Alphonce.

Aliongeza anawashauri Watanzania wasisite kucheza kwa wingi kwa sababu Jackpot ya SportPesa ni halali, kinachotakiwa wacheze kwa umakini kwa kiasi ambacho wanaweza kukipoteza ili wasije wakashindwa kulisha familia.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, alisema inahamasisha kuona sisi kama SportPesa tunaendelea kubadilisha maisha ya watu kila siku.

"Niwakumbushe Watanzania Jackpot ipo na itaendelea kuwapo kila wiki kutegemeana na lini haswa inatoka. Endeleeni kutuamini kama ambavyo Alphonce ametuamini na matokeo ya ushindi mtayapata," alisema Sabrina.

# *Silaha mpya yanukia Simba*

INATOKA UKURASA 24

Taarifa zaidi zinasema katika kuunda kikosi imara na chenye ushindani zaidi, huenda klabu hiyo ikaachana na baadhi ya wachezaji wake akiwamo Mrundi Saido Ntibazonkiza, Luis Miquissone, Mgambia Jobe Pa Omar, Freddy Michael, Babacar Sarr na Mkongomani Henock Inonga.

„Bado kuna wingu katika usajili wa Aishi Manula, kuna mambo mengi yanaendelea, kubakia au kuondoka Simba iko mikononi kwake mchezaji, atakavyoamua, kama fedha anazotaka atapewa.



Hilo ni panga la awamu ya kwanza, pia kuna panga lingine ambalo litawahusisha zaidi wachezaji wazawa, lengo ni kusajili nyota wengine wenye viwango vya juu ili kuirudisha timu hiyo kwenye makali yake yaliyozoeleka," kiliongeza chanzo che-

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ni kweli kikosi chao kinahitaji marekebisho makubwa kwa ajili ya kurejesha heshima. Ahmed amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kutulia wakati huu ambao viongozi wao ‚wanahaha' kuandaa kikosi ‚tishio' cha msimu ujao.

„Tunajua kipindi hiki mambo yatakuwa mengi na tutasikia taarifa nyingi za usajili, Simba tutafanya usajili mkubwa sana safari hii, ila ni nani, anatoka wapi, na majina yao, tutautangaza pale tutakapoona inafaa kupitia vyombo vyetu," Ahmed alisema.

Simba imemaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024 katika nafasi ya tatu, nyuma ya mabingwa, Yanga na Azam FC zote za Dar es Salaam.

Michezo
Jumamosi Juni 1, 2024
Nipashe



Grealish 'aliamsha' Man City UK. 22



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji Indonesia itakayochezwa kesho nchini humo. **PICHA: TFF**

# Silaha mpya yanukia Simba

## ●●● Ni winga Mpanzu kutoka AS Vita, mchakato wake wafikia pazuri...

**Na Adam Fungamwango**

KAZI iendelee, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi umetajwa uko katika hatua za mwisho za kumsajili winga wa kulia kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo (DRC), Elie Mpanzu, imeelezwa.

Habari za ndani zinasema mazungumzo kati ya Simba na Mpanzu yanaendelea vyema na baadhi ya makubaliano kati ya winga na klabu hiyo yameshafanyika ili mchezaji huyo aje kuichezea timu yake mpya.

Chanzo chetu kiliendelea kusema Simba imedhamiria kuboresha kikosi chake baada ya kutokuwa na matokeo mazuri katika msimu uliopita ambapo ilimaliza kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na pia ikiishia hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

„Ni kweli huyu mchezaji tumezungumza naye na mambo yanakwenda vizuri, ambacho watu hawaelewi ni alikuwa chaguo letu hata msimu uliopita lakini tulimkosa, msimu huu tumekwenda na dhamira moja kwa sababu tunataka kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi chetu, mambo yanakwenda vizuri vimebaki vitu vichache tu ili kumalizana,“ kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza benchi la ufundi la Simba linaamini usajili wa mchezaji huyo mwenye miaka 22, ambaye amepachika mabao 11 kwenye Ligi Kuu ya DRC msimu huu ukikamilika, utakuwa usajili wa kwanza wa klabu hiyo kwa wachezaji wa kigeni.

Chanzo hicho kilisema pia Simba inatajwa kumwania, Derrick Fordjour, kutoka Medeama ya Ghana pamoja na straika wa Red Arrows ya Zambia, Ricky Banda.

„Kuna Banda (Ricky), mwingine huenda akatua Simba msimu ujao, ni moja ya wachezaji waliofanya vyema katika Ligi ya Zambia msimu huu unaomalizika, mazungumzo yanaenda vyema na anaweza kumwaga wino wakati wowte,“ kilisema chanzo hicho.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga SC, Azam FC tambo zatawala

**Na Faustine Feliciane**

KOMBE ni letu, hayo ni maneno ya Yanga kuelekea mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa New Amaan Complex ulioko Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi kuelekea mchezo huo wa fainali yamekamilika na kikosi chao kimejipanga kukamilisha hesabu za msimu huu.

Kamwe alisema Yanga imeenda Zanzibar na ajenda mbili muhimu na wanaamini watapambana ili kuhakikisha wanafikia malengo yao.

„Tuna ajenda mbili katika mechi hiyo, moja ni kuutetea ubingwa wetu tuliouchukua msimu uliopita, namba mbili ni kulipa kisasi dhidi ya Azam FC ambao walitufunga mabao 2-1 katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu,“ alisema Kamwe.

Naye Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria ‚Zaka Zakazi‘ alisema malengo ya timu yao ni kutwaa ubingwa wa mashindano hayo yanayodhaminiwa na Benki ya CRDB.

„Malengo yetu ni kufanya vyema na kulibeba kombe hili ili kuendelea kuwapa burudani mashabiki na wanachama wetu katika msimu huu, „alisema Zakaria.

Ofisa huyo alisema wachezaji wote wana morali ya hali ya juu ingawa wamejiandaa kukutana na upinzani katika mechi hiyo muhimu na kubwa.

Aliongeza baada ya kumaliza mechi hiyo ya fainali, uongozi utaanza kutangaza majina ya wachezaji ambao itaachana nao

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >